SEPTEMBA 21, 2026
/islamicftz
Rabi ul-Thani 8 1448
VISION 2050
# IMAAN
Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah
ISSN 5618 - NO. 602



Mwinyi amteua Othman Makamu wa Rais, afungua sura mpya Zanzibar

# Kisima chaleta ahueni Hospitali ya Rufaa Njombe

■ Kilio cha maji kwa wagonjwa na watumishi kimepata jibu baada ya taasisi The Islamic Foundation kuchimba kisima cha mita 200



**MIMBARI ZETU**

Sheikh Dkt. Bandar Baleelah, Msikiti Mtakatifu wa Makka

Sheikh Muhammad, Masjid Nurah, Msamvu

Msikiti wa Al-Aqsa, Jerusalem

**Mwinyi asifu madrasa kama nguzo ya malezi ya jamii**

**Tofauti za fatwa zaleta mgongano sarafu za kidijitali nchi za Kiislamu**



## Nchemba: Dira 2050 sasa ni kazi, si karatasi

## Naibu Meya Moro: Serikali yatambua mchango wa The Islamic Foundation katika elimu



Naibu Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mohammed Mdeng'o akiteta jambo na Mwenyekiti wa The Islamic Foundation, Aref Nahdi



**Abbas kuhutubia UN kwa video; EU yashinikiza Marekani impe viza**

إنا لله وإنا إليه راجعون

# Muadhini Msikiti Mtakatifu Makka afariki baada ya kuadhini Alfajiri



Muadhini wa Msikiti Mtakatifu wa Masjid Al-Haram, Makkah, Sheikh Ibrahim bin Adel Al-Madani, amefariki dunia leo, Jumatatu, Septemba 21, 2026, akiwa na umri wa miaka 51, saa chache baada ya kutoa adhana yake ya mwisho ya Alfajiri.

Kwa mujibu wa magazeti ya Saudi Gazette na Okaz, kifo cha Sheikh Al-Madani kimethibitishwa pia na kituo cha televisheni cha Saudi Arabia, Al-Ekhbariya, huku taarifa hiyo ikisambaa katika vyombo mbalimbali vya habari na mitandao ya kijamii.

Mtandao wa Inside the Haramain ulitangaza kifo chake na kusambaza video inayomuonesha akiadhini Alfajiri, saa chache kabla ya kufariki dunia.

Sheikh Al-Madani alikuwa miongoni mwa waadhini wa Masjid Al-Haram wanaopokezana kutoa adhana za swala tano za kila siku.

Alianza kazi ya uadhini akiwa na umri wa miaka 15 katika msikiti mmoja wa Madina, kabla ya kuteuliwa kuwa muadhini wa Masjid Al-Haram mwaka 2018.

Alifahamika kwa sauti yake ya kipekee, iliyokuwa ikisikika katika adhana za kila siku na kuwavutia waumini waliokuwa wakitekeleza ibada katika msikiti huo.

Katika mahojiano aliyowahi kufanya, Sheikh Al-Madani alieleza jinsi alivyoshindwa kuzuia machozi alipotoa adhana yake ya kwanza katika Masjid Al-Haram, huku akiwaona waumini wakitufu Al-Kaaba.

Kwa mujibu wa taarifa za vyombo vya habari vya Saudi Arabia, swala ya jeneza lake ilipangwa kufanyika baada ya swala ya Alasiri katika Masjid Al-Haram, kabla ya kuzikwa katika makaburi ya Al-Mualla, Makka.

Kifo chake kimeibua salamu za rambirambi kutoka kwa waumini mbalimbali, huku video za adhana zake zikisambazwa mitandaoni kwa ajili ya kumuenzi.

Hadi wakati wa kuandaa habari hii, sababu mahususi ya kifo chake haikuwa imetangazwa rasmi

MWANDISHI WETU

# Dkt Mwigulu Nchemba: Dira 2050 sasa ni kazi, si karatasi

**Waziri Mkuu Nchemba ametaja vipaumbele vinane vya kuifanya Dira 2050 ionekane katika maisha ya wananchi, akisisitiza utekelezaji, uwajibikaji, ajira na ukuaji shirikishi wa uchumi.**

Serikali imeainisha vipaumbele vinane vya kimkakati inavyosema vitakuwa nguzo muhimu katika kufanikisha malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, huku wapangaji wakitakiwa kuelekeza nguvu zaidi katika utekelezaji, uwajibikaji na matokeo yanayopimika.

Vipaumbele hivyo vilitolewa na Waziri Mkuu, Dk Mwigulu Nchemba, wakati wa Mkutano wa Kitaifa wa Wapangaji uliofanyika Arusha, Septemba 16 na 17, 2026.

Kipaumbele cha kwanza ni kuoanisha sera, mipango na bajeti, ili kuhakikisha vipaumbele vya kitaifa vinaelekea katika mwelekeo mmoja. Dk Nchemba alisema wapangaji wanapaswa kuhakikisha miradi mikubwa ya kimkakati inakamilika kwa wakati, ndani ya gharama zilizopangwa na kwa viwango vinavyotarajiwa.

"Serikali imeimarisha uoanishaji wa sera, mipango na bajeti ili taasisi zote zitekeleze vipaumbele vya kitaifa kwa mwelekeo mmoja," alisema.

Kipaumbele cha pili ni utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP IV), unaohusu kipindi cha 2026/27 hadi 2030/31 na ambao ni awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Dira 2050.

Mpango huo unalenga kuunga mkono azma ya Tanzania kujenga uchumi wenye thamani ya dola trilioni moja na kuongeza wastani wa kipato cha mtu mmoja kwa mwaka hadi dola 7,000 ifikapo mwaka 2050.

Serikali pia imeweka mkazo katika ukuaji shirikishi wa uchumi na utulivu wa bei. Dk Nchemba alisema uchumi ulikua kwa asilimia 5.9 mwaka 2025, kutoka asilimia 5.6 mwaka 2024, huku mfumuko wa bei ukiendelea kubaki ndani ya lengo la asilimia tatu hadi tano.

"Wapangaji wanapaswa kuhakikisha mipango yao inachochea ukuaji huu zaidi na kuufanya uwe shirikishi katika ngazi zote," alisema.

Kipaumbele cha nne ni kupanua wigo wa kodi za ndani, ambapo Serikali inalenga kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Rais ya Maboresho ya Kodi ili kuongeza mapato ya ndani kwa ajili ya programu za maendeleo na kupunguza utegemezi wa vyanzo vya nje.

Kipaumbele cha tano ni kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa, uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa fedha za umma na miradi ya maendeleo. Dk Nchemba aliwataka wapangaji kuzingatia mapendekezo ya taasisi za usimamizi, udhibiti na kupambana na rushwa.

Kipaumbele kingine ni kutatua migogoro ya ardhi na kuboresha mipango ya matumizi ya ardhi, hatua ambayo Serikali inaiona kuwa muhimu katika kuwezesha uwekezaji katika kilimo, mifugo, viwanda na makazi.

Kipaumbele cha saba ni kuongeza ajira na ujuzi kwa vijana, hasa kwa kuoanisha mafunzo na mahitaji ya soko la ajira pamoja na mabadiliko ya teknolojia.

Cha nane ni kuimarisha uchumi wa buluu na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, maeneo ambayo Serikali inayaona kuwa na fursa za ubunifu, ukuaji wa uchumi, ulinzi wa mazingira na maendeleo endelevu.

Dk Nchemba alisema kipimo cha mwisho cha mafanikio ya Dira 2050 hakitakuwa wingi wa mipango na nyaraka zinazozalishwa, bali athari zake katika maisha ya wananchi.

"Wananchi hawatapima mafanikio yetu kwa uzuri na wingi wa nyaraka tulizoandika. Watayapima kwa ajira zilizozalishwa, ongezeko la kipato, huduma bora, kupungua kwa gharama, kuongezeka kwa uzalishaji na fursa zaidi kwa wananchi," alisema.



NA MWANDISHI WETU

# Kisima chaleta ahuweni ya maji Hospitali ya Rufaa Njombe



Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa Njombe, Daktari Gilbert Kwesi, amesema, ili kuendesha shughuli zake kwa ufanisi mahitaji ya maji hospitalini hapo ni lita 400,000 ilhali kiasi kilichokuwa kikipatikana ni lita 125,000 pekee kwa siku. Alisema kisima hicho ni muhimu katika kukabiliana na upungufu huo.

Kilio cha maji katika Hospitali ya Rufaa Njombe kimepata majibu baada ya taasisi ya The Islamic Foundation yenye makao yake makuu Morogoro kuchimba kisima cha mita 200.

Sambamba na kisima, taasisi hiyo imejenga msikiti kwa ajili ya wagonjwa, watumishi na jamii kwa ujumla. Kisima hicho kimefadhiliwa na Muneera Bint Abdullah Al-Fayyad kutoka Qatar.

Taasisi hiyo inayoongozwa na Aref Nahdi imetekeleza mradi huo hospitalini hapo ili kuondoa changamoto ya upatikanaji wa maji, inayowakabili wagonjwa, watumishi na jamii kwa ujumla inayofika hospitalini hapo kwa sababu mbalimbali.

Ukiacha kuwa ni hitaji muhimu katika matibabu, maji pia yanatumika katika usafi wa mazingira na matumizi ya siku hadi siku katika maisha ya watu kwa ajili ya kunywa, kuogea, kufulia, kupikia na kadhalika.

Kwa mujibu wa Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa Njombe, Daktari Gilbert Kwesi, ili kuendesha shughuli zake kwa ufanisi mahitaji ya maji hospitalini hapo ni lita 400,000 ilhali kiasi kilichokuwa kikipatikana ni lita 125,000 pekee kwa siku. Alisema kisima hicho ni muhimu katika kukabiliana na upungufu huo.

"Upatikanaji wa kisima hiki kwa sehemu kubwa unaenda kutusaidia kutatua changamoto mbalimbali za maji. Maji haya yamekuwa msaada mkubwa kwa wateja wetu na pia kwa wagonjwa lakini kwa watumishi ambao wanaishi eneo hili na matumizi mengine ya hospitali," alisema Dkt Kwesi.

Kisima hicho ni zaidi ya chanzo cha maji, bali ni chemchem ya matumaini kwa jamii hiyo, hasa katika mazingira ambayo maji ni hitaji la msingi katika usafi, afya na utoaji wa huduma za matibabu.

## Msikiti nao wajengwa

Mbali na kuchimba kisima, The Islamic Foundation imejenga msikiti ndani ya eneo la Hospitali ya Rufaa Njombe, hatua inayolenga kuwawezesha wagonjwa, watumishi na jamii inayozunguka hospitali kupata huduma za ibada kwa urahisi.

"Tunashukuru The Islamic Foundation kwa kusogeza huduma za kiroho kwa kutujengea msikiti ambao utasaidia sio tu wagonjwa bali pia watumishi ambao wamekuwa kila siku za Ijumaa wanasafiri kwenda mjini," alisema Dkt Kwesi. Ujenzi wa msikiti huo unaongeza sura ya kiroho katika mradi huo wa kijamii, ukizingatia kuwa katika Uislamu, kuwasaidia wenye mahitaji na kuwezesha watu kupata mahitaji ya msingi ni miongoni mwa matendo yenye thamani kubwa.

Kwa mtazamo wa Kiislamu, kutoa maji kwa wenye uhitaji ni miongoni mwa aina za sadaka jariyah, kwa kuwa manufaa yake yanaendelea kuwafikia watu wengi kila uchao.

## Zaidi ya visima 3,000

Tangu The Islamic Foundation isajiliwe rasmi nchini Tanzania mwaka 1998, taasisi hiyo imechimba zaidi ya visima 3,000 virefu na vifupi vya mkono, katika mikoa mbalimbali ya Tanzania ikiwa ni sehemu ya huduma za kijamii inazotoa, nyingine ikiwa ni matibabu, elimu, misaada ya dharura nk.

The Islamic Foundation inatekeleza miradi yake kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje, huku huduma zikitolewa kwa Watanzania bila ubaguzi wa kidini, kabila au mwelekeo wa kisiasa.

## Uchimbaji kisima, sambamba na ujenzi wa msikiti kwa ajili ya wagonjwa, watumishi na jamii kwa ujumla Hospitali ya Rufaa Njombe kwa ufadhili wa Muneera Bint Abdullah Al-Fayyad kutoka Qatar.







MWANDISHI WETU

# Mwinyi asifu madrasa kama nguzo ya malezi ya jamii



RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amesisitiza umuhimu wa madrasa katika kujenga msingi imara wa malezi na kizazi chenye maadili mema.

Aidha, alitoa wito kwa wazazi, walimu na viongozi wa dini kushirikiana katika kuwalea watoto na vijana.

Rais Dkt. Mwinyi ametoa kauli hiyo Septemba 18, 2026 katika dua ya kuliombea Taifa, hususan kumuomba Mwenyezi Mungu aiepushe Zanzibar na madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na mvua kubwa pamoja na athari za El Niño.

Akizungumza katika hafla hiyo iliyofanyika katika Almadrasat Swifat Nabawiyatil Karimah iliyopo Msolopa Kilimani, Mkoa wa Mjini Magharibi, Dkt. Mwinyi alisema madrasa zina nafasi muhimu katika malezi ya watoto hasa katika kuwajengea tabia njema, nidhamu na hofu ya Mwenyezi Mungu.

Kuhusu umuhimu wa ushirikiano katika malezi, Dkt, Mwinyi alisema inasaidia kukabiliana na changamoto za kimalezi zinazotokana na matumizi ya vifaa vya teknolojia za mawasiliano - ikiwemo simu janja na mitandao ya kijamii – ambayo imefungua mlango wa taarifa nyingi baadhi zikiwa na madhara kimaadili.

Kwa msingi huo, Mwinyi alisema ufanisi katika malezi utategemea ushirikiano wa pande ne muhimu: walimu wa madrasa, wazazi/ walezi, viongozi wa dini na jamii kwa ujumla

Lakini kipekee, Mwinyi alihimiza wazazi kuwa karibu na watoto wao, kuwafuatilia na kuwaongoza katika matumizi sahihi ya teknolojia, huku wakihakikisha wanapata malezi yanayojenga utu, heshima na uwajibikaji.

Katika hatua nyingine, Rais Dkt. Mwinyi aliwataka wananchi kuendelea kudumisha umoja, mshikamano na amani, lakini pia aliwahimiza kuchukua tahadhari dhidi ya mvua kubwa zinazotarajiwa na kuzingatia taarifa pamoja na maelekezo yanayotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Serikali.

NA MWANDISHI WETU

# NAIBU MEYA MORO: Serikali yatambua mchango wa The Islamic Foundation katika elimu




**Akizungumza katika Mahafali ya 20 ya Shule ya Msingi Imaan iliyopo Kilakala, Morogoro Mjini, Mdeng'o alisema mchango wa taasisi hiyo umekuwa muhimu katika kuunga mkono juhudi za Serikali za kujenga taifa lenye wananchi wenye maarifa, maadili na uwezo wa kuchangia maendeleo.**

Naibu Meya wa Manispaa ya Morogoro, Mohammed Mdeng'o, ameipongeza Taasisi ya The Islamic Foundation kwa ushiriki wake katika kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi. Aidha ameisifu mchango wake katika sekta ya elimu.

Akizungumza katika Mahafali ya 20 ya Shule ya Msingi Imaan iliyopo Kilakala, Morogoro Mjini, Mdeng'o alisema mchango wa taasisi hiyo umekuwa muhimu katika kuunga mkono juhudi za Serikali za kujenga taifa lenye wananchi wenye maarifa, maadili na uwezo wa kuchangia maendeleo.

Alisema Serikali inatambua kuwa uwekezaji katika elimu ni muhimu katika kuandaa kizazi chenye uwezo wa kutoa huduma za kijamii bila ushirikiano na wadau mbalimbali.

Kwa msingi huo, Mdeng'o alitoa trai kwa taasisi, mashirika na wadau wengine kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuanzisha na kutekeleza miradi inayolenga kuboresha maisha ya wananchi.

Naibu Meya huyo alisema mchango wa The Islamic Foundation katika elimu unapaswa kuendelea kupewa nafasi, kwa kuwa elimu inayotolewa kwa kuzingatia taaluma na maadili huwasaidia watoto kukua wakiwa na maarifa, nidhamu na uwezo wa kushiriki katika ujenzi wa jamii.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Taasisi ya The Islamic Foundation, Aref Nahdi, amesema taasisi hiyo itaendelea kutekeleza wajibu wake wa kusaidia jamii katika nyanja mbalimbali, ikiwemo kuwekeza katika sekta ya elimu.

Mwenyekiti Nahdi alisema uwekezaji huo haulengi tu kuwapatia watoto maarifa ya kitaaluma, bali pia kuwajengea misingi ya malezi inayozingatia maadili mema ya Kiislamu, ili wahitimu waweze kuwa sehemu ya kizazi kinachotambua wajibu wake kwa jamii na taifa.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa The Islamic Foundation, Sheikh Ibrahim Twaha, amewataka wahitimu wa Shule ya Msingi Imaan kuendelea kuyazingatia maadili na misingi waliyojifunza wakati wa masomo yao, akisisitiza kuwa elimu inapokuwa na maarifa pekee bila tabia njema na uwajibikaji, haikamilishi kikamilifu jukumu la kumjenga mwanafunzi.

Sheikh Ibrahim alisema wahitimu wanapaswa kutumia elimu waliyoipata kama msingi wa kufikia hatua nyingine za masomo na maisha, huku wakibeba pamoja nao nidhamu, heshima, uwajibikaji na maadili mema.

Awali, katika risala yao, wahitimu walikiri kuwa wamepewa msingi mzuri wa kitaaluma, kimaadili na stadi mbalimbali zitakazowasaidia kujitegemea na kuchangia maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla.

Risala hiyo imeeleza kuwa elimu na malezi waliyoyapata ni msingi wa maandalizi ya hatua nyingine ya maisha, huku wakitambua umuhimu wa kutumia maarifa waliyojifunza kwa manufaa yao na jamii inayowazunguka.

ربيع ثان




# MATUKIO KATIKA PICHA

Na abdulrahman Omar

0655 763 580

## Mahafali ya 20 ya Shule ya Msingi Imaan iliyopo Kilakala, Morogoro















# MIMBARI ZETU

**IMEANDALIWA**
**Na Barnabas Mkwayu**
**0766 364 354**

## KUTOKA

Masjid Nurah
**(Msamvu, Morogoro)**

Masjid Al-Haram
**(Makka)**

Msikiti wa Al-Aqsa
**(Jerusalem)**



## MSIKITI MTAKATIFU, MAKKA



# Imamu wa Makka aonya dhidi ya dhana mbaya

**MAKKA:** Imamu wa Msikiti Mtakatifu wa Makka, Sheikh Dkt. Bandar Baleelah, amewataka Waislamu kuacha kuwadhania wenzao vibaya, akisema dhana mbaya inaweza kuwa chanzo cha upelelezi wa mambo ya watu, masengenyo, chuki na uadui katika jamii.

Katika Khutba ya Ijumaa, Septemba 18, 2026, Sheikh Baleelah alisema dhana mbaya huingiza wasiwasi, huzuni na migogoro katika nyoyo za watu, wakati kuwadhania wengine kwa wema kunachangia utulivu wa nafsi, amani na kuimarika kwa uhusiano wa kijamii.

Alisisitiza kuwa Muislamu anatakiwa kujenga tabia ya kuwadhania ndugu zake kwa wema na kutafuta udhuru pale anapoona jambo linaloweza kutafsiriwa kwa namna tofauti.

Sheikh Baleelah alisema wajibu huo unapaswa kuzingatiwa katika familia, ujirani, sehemu za kazi na katika jamii kwa ujumla, kwa kuwa dhana zisizo na msingi zinaweza kuharibu mahusiano na kusababisha migogoro isiyokuwa na sababu.

Aidha, aliwataka waumini kuepuka mazingira yanayoweza kuzua mashaka yasiyo ya lazima, huku akiwashauri kutoa ufafanuzi mapema pale wanapotambua kuwa matendo au maneno yao yameeleweka vibaya.

Kwa mujibu wa Sheikh Baleelah, Muislamu hapaswi kujenga hukumu juu ya mtu mwingine kwa kutegemea hisia, uvumi au tafsiri zisizo na ushahidi, bali anatakiwa kuwa mwangalifu katika kuhifadhi heshima na utu wa wengine.

Akizungumzia usalama wa maeneo matakatifu, Sheikh Baleelah pia alilaani mashambulizi yanayohusishwa na kundi la Houthi dhidi ya Saudi Arabia, hususan vitisho vinavyolenga Makka na Madina.

Alisema kulenga maeneo matakatifu, misikiti, shule na mali za wananchi ni kinyume na misingi ya dini na ubinadamu, akisisitiza kuwa kuwatisha waumini na kuhatarisha maisha ya watu wasio na hatia hakukubaliki.

Sheikh Baleelah alihitimisha kwa kuhimiza Waislamu kudumisha mshikamano, kuheshimiana, kulinda amani na kuhakikisha maeneo matakatifu yanaendelea kuwa salama kwa waumini.

## MASJID NURAH, MSAMVU



# Sheikh Abdulrahman aasa mcheni Allah hata mkiwa faraghani

**MOROGORO:** Waislamu wametakiwa kumcha Mwenyezi Mungu na kutambua kuwa hakuna jambo wanalolifanya kwa siri linaloweza kufichika mbele Yake, kwa kuwa Yeye Anaona, Anasikia na Anajua kila kitu.

Ujumbe huo umetolewa na Sheikh Abdulrahman Muhammad katika Khutba ya Ijumaa, Septemba 18, 2026, iliyofanyika Masjid Nurah, Msamvu, Morogoro, iliyobeba mada: "Alam ya'lam bi annallaha yara" — "Je, hajui ya kwamba Mwenyezi Mungu anaona?"

Sheikh Muhammad alisema mwanadamu anaweza kujificha ndani ya hoteli, katika mji wake, vichakani au mapangoni, lakini hawezi kujificha mbele ya Mwenyezi Mungu, iwe ametenda jambo hilo hadharani au kwa siri.

Akirejea maelezo ya Imam Shaukan (Allah amrehemu), Sheikh huyo alisema Mwenyezi Mungu anazijua hali zote za mwanadamu, jambo ambalo linapaswa kumfanya Muislamu kuwa na taqwa, kujiepusha na maasi na kuishi kwa uadilifu wakati wote.

Alikumbusha kauli ya Qur'an: "Wa huwa maakum aina maa kuntum" — "Na Yuko pamoja nanyi popote mlipo."

Alisema kutambua kwamba Mwenyezi Mungu anamuona na anajua siri zake zote ni msingi muhimu wa kujenga moyo wenye hofu ya Allah, uaminifu, unyenyekevu na tabia njema.

Sheikh Muhammad alisema hofu ya Mwenyezi Mungu haipaswi kuonekana wakati mtu yupo mbele ya watu pekee, bali inapaswa kuwa sehemu ya maisha yake hata akiwa peke yake.

Kwa msingi huo, aliwataka Waislamu kutofanya dhambi kwa kujidanganya kuwa hakuna anayewaona, akisisitiza kuwa Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yote, Anayejua yaliyofichika na yaliyo wazi. Aidha, aliwahimiza waumini kujenga maisha yanayoongozwa na kumcha Allah, kwa kuwa kutambua uwepo na uangalizi Wake kunamkinga mwanadamu na maovu na kumsaidia kushikamana na mema.

# Maelfu waswali Al-Aqsa licha ya vikwazo vya Israel



Makumi ya maelfu ya Wapalestina wameswali Ijumaa katika Msikiti wa Al-Aqsa, Jerusalem, licha ya vizuizi vikali vilivyowekwa na vikosi vya Israel katika maeneo yanayouzunguka msikiti huo.

Kwa mujibu wa Shirika la Habari la Jordan (Petra), Idara ya Waqf ya Jerusalem imethibitisha kuwa makumi ya maelfu ya waumini walihudhuria swala hiyo.

Shirika la Habari la Palestina (WAFA) limeripoti kuwa vikosi vya Israel vilimkamata kijana mmoja ndani ya viwanja vya Al-Aqsa wakati khutba ikiendelea.

Vikosi hivyo pia vilizuia baadhi ya watu wenye ulemavu wanaotumia viti vya magurudumu kufika msikitini.

Aidha, viliimarisha ulinzi kwenye milango ya mji wa kale na kukagua vitambulisho vya waumini, huku baadhi wakizuiwa kuingia.

Vyanzo: Petra na WAFA

MWANDISHI WETU

# Mwinyi amteua Othman makamu wa rais, afungua sura mpya Z'bar

Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) imeanza rasmi sura mpya baada ya Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Mwinyi, kumteua tena Othman Masoud Othman (OMO) kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, hatua inayorejesha ACT-Wazalendo serikalini baada ya kukaa nje kwa muda mrefu.

Uteuzi huo ulianza rasmi jana na Othman anatarajiwa kuapishwa kesho kutwa saa 4:00 asubuhi katika Ikulu ya Zanzibar, kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi, Mansura Mosi Kassim.

Uteuzi huo unafungua ukurasa mpya katika utekelezaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, huku wadau wa siasa wakieleza kuwa hatua inayofuata ni kuona namna viongozi wa CCM na ACT-Wazalendo watakavyotekeleza makubaliano yao na kushughulikia changamoto zilizokuwapo.

Hii ni mara ya pili kwa Othman kushika nafasi hiyo. Aliteuliwa kwa mara ya kwanza Machi 1, 2021, kufuatia kifo cha aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, aliyefariki Februari 17, 2021.

Uteuzi wa sasa umefuatia ACT-Wazalendo kuwasilisha rasmi jina la Othman kwa Rais Mwinyi juzi, kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya Zanzibar kupitia Marekebisho ya 10 ya mwaka 2010.

Kwa mujibu wa Katiba hiyo, chama cha siasa kinachoshika nafasi ya pili katika uchaguzi mkuu na kupata zaidi ya asilimia 10 ya kura kina haki ya kutoa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar.

Hata hivyo, utekelezaji wa matakwa hayo ulikuwa umekwama kwa takribani miezi 11 tangu uchaguzi mkuu wa Oktoba 29, 2025, kutokana na sababu mbalimbali za kisiasa.

Safari ya maridhiano

Hatua ya sasa imefikiwa baada ya mchakato mrefu wa mazungumzo na maridhiano ya kisiasa ulioanza Novemba mwaka jana, ambapo pande zinazohusika zilifikia tamko la pamoja lililoweka misingi ya kushughulikia kero za kisiasa na kuimarisha maridhiano Zanzibar.

Baada ya tamko hilo, iliundwa kamati ya pamoja iliyopangiwa kusimamia utekelezaji wa makubaliano, ikiwamo mchakato wa uteuzi wa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka ACT-Wazalendo.

Baada ya kukaa nje ya SUK kwa muda mrefu, ACT-Wazalendo hatimaye iliwasilisha jina la Othman kwa Rais Mwinyi, hatua iliyowezesha uteuzi huo kufanyika rasmi.

Akizungumzia hatua hiyo, Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM Zanzibar, Khamis Mbeto, aliipongeza ACT-Wazalendo kwa kuwasilisha jina hilo kwa mujibu wa Katiba na Rais Mwinyi kwa kuliteua.

"CCM inakipongeza Chama cha ACT-Wazalendo kwa kufikiria kwa wigo mpana na kukubali kurejea serikalini baada ya kukaa nje kwa muda mrefu," alisema. Mbeto alisema CCM itatoa ushirikiano kwa SUK katika kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi.

Hata hivyo, alisisitiza kuwa ilani inayotekelezwa na Serikali ni ya CCM, huku Makamu wa Kwanza wa Rais akitekeleza majukumu atakayopangiwa na Rais kwa mujibu wa Katiba.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa nchini, Juma Khatib, aliipongeza Serikali kwa kutekeleza matakwa ya Katiba ya Zanzibar, huku akizisifu CCM na ACT-Wazalendo kwa kufikia muafaka.

"Tulikuwa na mkwamo mkubwa wa kisiasa, lakini hii ni hatua kubwa kwani ni kutekeleza matakwa ya Katiba na sheria," alisema Khatib.





UKHTI FATIMA SS




# Benki ya Kiislamu yatajwa katika tatu bora orodha ya Forbes

Benki ya Kiislamu ya Qatar (QIB) imeshika nafasi ya tatu duniani katika kundi la benki za ukubwa wa kati wa juu, kwenye orodha ya Forbes ya benki zilizofanya vizuri zaidi mwaka 2026.

Kwa mujibu wa Gulf Times la Septemba 19, mafanikio hayo yanatokana na matokeo ya kifedha ya QIB, yanayoonyesha ukuaji wa faida, mali na amana za wateja.

Takwimu za mwaka ulioishia Desemba 31, 2025, zinaonyesha benki hiyo ilipata faida halisi ya riyal bilioni 4.83, ongezeko la asilimia tano ikilinganishwa na mwaka uliotangulia.


Mali zake ziliongezeka kwa asilimia 10.1 hadi riyal bilioni 221.1, huku amana za wateja zikikua kwa asilimia 14.2 na kufikia riyal bilioni 142.7.

QIB pia ilirekodi uwiano wa gharama kwa mapato wa asilimia 16.3, kiwango bora zaidi katika sekta ya benki nchini Qatar, huku uwiano wa mtaji ukifikia asilimia 22.2.

Forbes, kwa kushirikiana na Statista, ilitathmini benki 500 kutoka nchi 89 kwa kuzingatia faida, ukuaji, uimara wa mtaji, ubora wa mali na ufanisi wa uendeshaji.

Benki ziligawanywa katika makundi sita kulingana na ukubwa wa mali zake, na QIB ikashika nafasi ya tatu katika kundi lake.

Mtendaji Mkuu wa QIB, Bassel Gamal, amesema mafanikio hayo yanaakisi uimara wa kifedha, nidhamu ya uendeshaji na mkakati wa muda mrefu wa benki hiyo.




## Wanazuoni wajielimishe kabla ya kuzungumzia huduma fedha za Kiislamu, wito

**Wanazuoni wa Kiislamu wametakiwa kuongeza uelewa wao kuhusu fedha za Kiislamu kabla ya kutoa elimu na ushauri kwa waumini kuhusu masuala ya kifedha.**

**Wito huo umetolewa nchini Nigeria na Mkurugenzi wa Elimu kwa Viongozi wa Shule ya Biashara ya Nungu, Dkt. Jubril Salaudeen, katika kongamano la wadau wa fedha za Kiislamu lililoandaliwa na Benki ya Hayat Trust Non-Interest Microfinance mjini Ijebu-Ode, jimbo la Ogun.**

**Kwa mujibu wa tovuti ya Muslim News Nigeria la Septemba 15, 2026, Salaudeen amesema Waislamu wengi huwategemea wanazuoni kupata mwongozo kuhusu masuala ya fedha, hivyo ni muhimu kwao kuelewa mfumo huo kwa kina ili kutoa ushauri sahihi.**

**Amesema fedha za Kiislamu ni taaluma maalumu inayohitaji uelewa wa kanuni, bidhaa na miamala yake, badala ya kutegemea maarifa ya jumla pekee.**

**Akifafanua misingi yake, Salaudeen amesema mfumo huo unakataza riba, gharar, ambayo ni kutokuwa na uhakika kupita kiasi katika miamala, na maysir, yaani kamari.**

## Malaysia, Indonesia mbioni kuanzisha baraza la halal la Asean

**Malaysia na Indonesia zinapanga kuanzisha Baraza la Halal la Jumuiya ya Mataifa ya Kusini-Mashariki mwa Asia (ASEAN), kwa lengo la kuimarisha ushirikiano na kuongeza nafasi ya kanda hiyo katika uchumi wa halal duniani.**

**Naibu Waziri Mkuu wa Malaysia, Ahmad Zahid Hamidi, amesema nchi hizo zinatarajia kuanzisha baraza la pamoja Desemba mwaka huu, kabla ya kuzindua baraza la kikanda Septemba 2027 nchini Malaysia.**

**Akizungumza katika Mkutano wa Halal 20 uliofanyika Jakarta, Septemba 18, 2026, Hamidi amesema baraza hilo litarahisisha utambuzi wa vyeti vya halal, kuoanisha viwango vya bidhaa na kupunguza vikwazo vya biashara miongoni mwa nchi wanachama.**

**Malaysia imejitolea kuwa sekretarieti ya baraza hilo, huku Indonesia ikipendekezwa kuwa mwenyekiti wake wa kwanza, kutegemea makubaliano ya wanachama.**

**Naibu Rais wa Indonesia, Gibran Rakabuming Raka, ameunga mkono mpango huo na kuhimiza utekelezaji wake kuharakishwa.**




# Tofauti za fatwa zaleta mgongano sarafu za kidijitali nchi za Kiislamu



Tofauti za tafsiri za Sharia kuhusu sarafu za kidijitali, maarufu kama cryptocurrency, zimeibua mitazamo tofauti katika nchi zenye mifumo ya fedha za Kiislamu, huku Malaysia na Falme za Kiarabu (UAE) zikiruhusu baadhi ya sarafu hizo na wanazuoni wa Pakistan wakizipinga.

Kwa mujibu wa ripoti ya Septemba 14, 2026, ya shirika la kimataifa la tathmini ya mikopo, Fitch Ratings, kukosekana kwa mwongozo mmoja wa Sharia kunafanya matumizi ya sarafu hizo kukua kwa kasi tofauti kati ya nchi.

Fitch inasema baadhi ya wanazuoni wanazikataa, wengine wanaziruhusu kwa masharti, huku benki nyingi za Kiislamu zikiendelea kuwa makini kutokana na hatari za kifedha na kutokubaliana kwa wanazuoni.

Kwa nini wanazuoni wanatofautiana?

Kiini cha tofauti hizo ni iwapo sarafu za kidijitali zinaweza kutambuliwa kama maal, yaani mali yenye thamani inayokubalika katika Sharia, na iwapo biashara yake inakidhi masharti ya miamala ya Kiislamu.

Nchini Malaysia, Baraza la Ushauri wa Sharia la Tume ya Masoko ya Mitaji liliamua mwaka 2020 kuwa sarafu za kidijitali zinazodhibitiwa na tume hiyo zinaweza kutambuliwa kama mali.

Baraza hilo linatofautisha sarafu zisizo na mali inayozidhamini na zile zinazodhaminiwa na dhahabu, fedha au sarafu za kawaida.

Sarafu zisizo na mali inayozidhamini zinachukuliwa kama bidhaa, si fedha kwa maana ya Sharia. Zinazodhaminiwa na dhahabu, fedha au sarafu zinapaswa kufuata masharti ya ubadilishaji wa fedha yanayojulikana kama bai al-sarf.

Kwa tokeni za uwekezaji, fedha zinazokusanywa na haki za wawekezaji lazima zizingatie Sharia. Uamuzi huo unahusu mali zinazodhibitiwa na tume, si sarafu zote duniani.

Kwa msingi huo, Malaysia imetambua Bitcoin, Ethereum, XRP na Stellar miongoni mwa sarafu zinazokidhi masharti ya Sharia katika mfumo wake wa udhibiti.

Falme za Kiarabu zimechukua mkondo mwingine. Fitch inasema Mamlaka Kuu ya Sharia ya Benki Kuu ya UAE iliruhusu miamala ya Bitcoin mwaka 2025.

Mwaka 2018, mamlaka nyingine ya masuala ya Kiislamu nchini UAE ilipinga miamala ya Bitcoin katika mazingira ya wakati huo, lakini ikaacha uwezekano wa hukumu kubadilika endapo sarafu hizo zingedhibitiwa na kukidhi masharti husika.

Uamuzi huo umeambatana na mfumo wa udhibiti wa mali za kidijitali unaoruhusu baadhi ya benki kutoa huduma za udalali na kuhifadhi sarafu hizo kwa wateja.

Hata hivyo, udhibiti wa kisheria na idhini ya Sharia ni mambo tofauti. Udhibiti unahusu leseni na usimamizi wa biashara, wakati idhini ya Sharia inahusu uhalali wa bidhaa na miamala yake kwa mujibu wa kanuni za Kiislamu.

Muhtasari wa Fitch haujafafanua kwa kina hoja za kifiqhi zilizotumika katika uamuzi huo. Hivyo, kuruhusiwa kwa Bitcoin hakupaswi kutafsiriwa kuwa UAE imeruhusu kila sarafu au kila aina ya biashara ya kidijitali.

Pakistan yapinga sarafu hizo

Nchini Pakistan, taasisi ya Darul Ifta ya Jamia Darul Uloom Karachi ilitoa fatwa Juni 10, 2026, iliyosainiwa na wanazuoni akiwamo Sheikh Muhammad Taqi Usmani.

Wanazuoni hao walisema sarafu za kidijitali hazitambuliki kama mali halali kwa mujibu wa tathmini ya wataalamu iliyopatikana hadi wakati huo. Kwa msingi huo, walihitimisha kuwa kuzitumia kununua bidhaa hakuruhusiwi, ikiwamo kupitia USDT, sarafu inayolenga kudumisha thamani inayolingana na dola ya Marekani.

Hata hivyo, Mamlaka ya Udhibiti wa Mali za Kidijitali ya Pakistan (PVARA) iliomba ufafanuzi zaidi. Ifahamike kuwa fatwa ya Pakistan ni maoni ya wanazuoni, na haiifanyi crypto kuwa haramu kisheria nchini Pakistan

Mwenyekiti wake, Bilal bin Saqib, amesema sarafu za kubahatisha bei zinapaswa kutofautishwa na tokeni zinazowakilisha dhahabu, sukuk au mali halisi.



SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

# Je ugonjwa ni udhuru unaokubalika wa kuacha Swala?

**Swali:** **Mtu alinunua kitabu, kisha akakuta kimeandikwa juu yake "waqf", afanye nini?**

**Jibu:** Aende kwa muuzaji na amueleze kuwa kitabu hicho ni waqf hivyo hakiruhusiwi kuuzwa. Hiyo ina maana mkataba wa mauziano unavunjika kwa sababu imebainika kuwa mauziano hayo hayakuwa sahihi. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

**Swali:** **Wagonjwa wengi hupuuza Swala na kusema: "Nikipona, nitaswali Swala nilizoacha" na wengine husema: "Nitaswalije hali ya kuwa siwezi kutawadha wala kujisafisha kutokana na najisi?" Je, mnawaelekezaje watu kama hawa?**

**Jibu:** Ugonjwa haumzuii mtu kutekeleza Swala. Kushindwa kutawadha si udhuru unaokubalika, maadamu bado ana akili yake. Ni wajibu kwa mgonjwa kuswali kwa kadiri ya uwezo wake. Mgonjwa anapaswa kutawadha kwa kutumia maji ikiwa ana uwezo wa kufanya hivyo lakini ikiwa hawezi atatayammamu na kuswali.

Pia, anatakiwa kuosha najisi iliyopo mwilini mwake au kwenye nguo zake wakati wa Swala, au abadilishe nguo zenye najisi na kuvaa nguo safi wakati wa Swala. Ikiwa hawezi kabisa kuosha najisi hiyo, wala hawezi kubadilisha nguo zenye najisi na kupata nguo safi, basi wajibu huo unaanguka kwake, naye ataswali kulingana na hali yake.

Haya ni kwa mujibu wa kauli ya Allah Mtukufu: "Basi mcheni Allah kwa kadiri ya uwezo wenu." [Qur'an, 64:16], na pia kwa mujibu wa kauli ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani): "Ninapowaamrisheni jambo, litekelezeni kwa kadiri ya uwezo wenu." [Bukhari na Muslim].

Katika hadith nyingine, Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alimwambia 'Imraan bin Husayn (Allah amridhie yeye na baba yake), alipomweleza kuhusu ugonjwa wake: "Swali ukiwa umesimama. Ikiwa huwezi, basi swali ukiwa umeketi. Ikiwa huwezi, basi swali ukiwa umelala kwa ubavu." [Bukhari, na pia An-Nasaa'i kwa isnadi sahihi, ambaye ameongeza: "Ikiwa huwezi [hata hivyo], basi swali ukiwa umelala chali." Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

**Swali:** **Mgonjwa alilazwa hospitalini kwa ajili ya kufanyiwa upasuaji tumboni kisha alikaa takribani siku moja na nusu akiwa hajitambui kutokana na athari za dawa ya usingizi (nusu kaputi). Baada ya kuzinduka, aliendelea kukaa kwa muda wa wiki moja akiwa hawezi kuinama ili kutekeleza Swala, wala hawezi kuoga mwili wake wote kwa ajili ya kujitwaharisha. Mtu huyu anatakiwa kuswali vipi?**

**Jibu:** Ni wajibu kwa mgonjwa kutekeleza Swala za faradhi kwa kadiri ya uwezo wake. Hii ni kutokana na kauli ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alipoulizwa na baadhi ya wagonjwa kuhusu jambo hili alisema: "Swali ukiwa umesimama. Ikiwa huwezi, basi swali ukiwa umekaa. Ikiwa huwezi, basi swali ukiwa umelala kwa ubavu" [Al-Bukhari]. Katika mapokezi ya An-Nasai ameongeza: "Ikiwa huwezi, basi swali ukiwa umelala chali."

Na pale fahamu zake zinapopotea kwa sababu ya dawa ya usingizi au kwa sababu ya ugonjwa, anapaswa kuzilipa Swala alizozikosa mara tu fahamu zake zinapomrudia, na azilipe kwa mpangilio, huku akifanya hivyo kwa haraka kulingana na uwezo wake.

Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani): "Mwenye kulala akaikosa Swala, au akaisahau, basi aiswali mara atakapoikumbuka. Hakuna kafara yake isipokuwa hiyo."

Kwa hiyo, hapana shaka kwamba mtu aliyepoteza fahamu kwa sababu ya ugonjwa au kwa sababu ya dawa ya usingizi kwa siku moja, mbili au tatu, hukumu yake ni kama mtu aliyelala.

Hapaswi kuchelewesha Swala alizozikosa mpaka muda wa Swala kama hizo ufike tena; bali anatakiwa kuanza kuzilipa mara tu fahamu zake zinapomrudia, kama mtu aliyelala anapokuwa ameamka, na kama mtu aliyesahau anapokumbuka.

Na ikiwa hawezi kutumia maji, basi tayammum itamtosheleza, kwa mujibu wa aya iliyotangulia. Na Allah ndiye Muwezeshi wa kupata tawfiki.

NA
Na Abeid Othman
0754 990 083

# Vijana wa Kiislamu, tafuteni fursa msikimbie nchi



**Kumekuwa na fikra inayozidi kukua kwa vijana we wengi, kwamba mafanikio ya maisha yanapatikana zaidi nje ya nchi - Ulaya, Marekani au Afrika Kusini. Anaona picha za maisha ya watu kwenye mitandao ya kijamii, anasikia simulizi za wanaodai kupata fedha nje, na hatimaye anaamini kwamba suluhisho la maisha yake ni kuondoka nchini.**

# Vijana wa Kiislamu, tafuteni fursa msikimbie nchi

Kumekuwa na fikra inayozidi kukua kwa vijana we wengi, kwamba mafanikio ya maisha yanapatikana zaidi nje ya nchi - Ulaya, Marekani au Afrika Kusini. Anaona picha za maisha ya watu kwenye mitandao ya kijamii, anasikia simulizi za wanaodai kupata fedha nje, na hatimaye anaamini kwamba suluhisho la maisha yake ni kuondoka nchini.

Lakini si kila anayehama nchini anapata mafanikio, kama ambavyo si kila anayebaki nchini anashindwa. Mafanikio hayafungwi na mipaka ya nchi pekee. Yanahitaji uamuzi, uthubutu, maarifa, juhudi, nidhamu na uwezo wa kutambua fursa zilizopo katika mazingira yanayokuzunguka.

Tanzania bado ina fursa nyingi. Kuna sekta ya kilimo, mifugo, uvuvi, biashara, usafirishaji, ujenzi, utalii, teknolojia, viwanda, huduma, ufundi na sekta nyingine nyingi.n Katika miji na vijiji kuna mahitaji ya bidhaa na huduma mbalimbali ambayo bado hayajapatiwa majibu ya kutosha.

Kijana anaweza kuanza kwa kile alichonacho. Si kila fursa inahitaji shahada ya chuo kikuu. Baadhi zinahitaji ujuzi, ubunifu, kujifunza na kuwa tayari kufanya kazi. Ufundi wa magari, umeme, useremala, ushonaji, upishi, ujenzi, saluni, kilimo cha kisasa, ufugaji, biashara ndogo, huduma za kidijitali na shughuli nyingine, zinaweza kuwa mwanzo wa safari ya kujenga maisha.

Kinachohitajika ni uthubutu na uamuzi wa kuanza. Wakati mwingine vijana wanapoteza muda wakisubiri kazi yenye mshahara mkubwa, ofisi nzuri na cheo kikubwa. Wakati huohuo, fursa ndogo zinazowazunguka zinapuuzwa.

## Hizi ni fikra potofu

Acheni kuamini kuwa maisha yapo Ulaya, Marekani au Afrika Kusini pekee kwani kila nchi ina gharama zake za maisha, ushindani wa ajira, sheria, changamoto za uhamiaji na mazingira ambayo mhamiaji anatakiwa kuyafahamu kabla ya kuamua kwenda.

Tumeona mfano mzuri wa vijana waliokwenda Afrika Kusini kwa matarajio makubwa lakini hivi karibuni wamerudi Tanzania bila mafanikio waliyotarajia. Miongoni mwa waliorudi wapo wenye majina na malezi ya Kiislamu.

Baadhi yao waliondoka wakiamini kwamba kule ndiko walikokuwa wakisubiriwa kupata maisha bora lakini wamerudi wakiwa wanechoka!

Hili si jambo la kuwadhihaki wala kuwahukumu waliorejea. Badala yake, liwe funzo kwa kizazi kinachofikiria kuondoka. Kwenda nje ya nchi si dhamana ya mafanikio.

Kama mtu anaenda bila ujuzi, bila kazi inayomsubiri, bila mtaji, bila taarifa sahihi na bila mpango wa maisha, anaweza kukutana na mazingira magumu zaidi kuliko aliyoyaacha.

Mitandao ya kijamii imeongeza tatizo hili. Kijana anaweza kuona mtu akiwa Dubai, London, Johannesburg au New York akiwa katika mazingira mazuri na kudhani maisha yote ya mtu huyo yako hivyo. Lakini picha moja haiwezi kueleza gharama ya maisha ya mtu mzima.

Vijana wa Kiislamu wanapaswa kujifunza kutofautisha kati ya kutafuta fursa na kukimbia matatizo. Kuna tofauti kubwa kati ya mtu anayehama akiwa na mpango wa kujenga maisha na mtu anayekwenda kwa matumaini kwamba akifika tu nchi nyingine fedha zitajitokeza. Kabla ya kufikiria kuhama, kijana ajiulize: Nina ujuzi gani? Ninaenda kufanya kazi gani? Nani atanisaidia nikifika? Nina gharama za kuanzia? Ninaelewa sheria za nchi hiyo? Nina mpango wa miaka miwili, mitatu au mitano? Kama majibu hayapo, huenda kinachohitajika kwanza si tiketi ya ndege, bali mpango wa maisha.

## Funzo la Hijra ya Mtume

Hijra Ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani) ilikuwa na mpango, si kubahatisha Hatua yake ya kuhama mji aliozaliwa wa Makka na kwenda Madina, ni funzo muhimu kuhusu imani, uamuzi, subira na pia maandalizi.

Hijra haikuwa kitendo cha kukurupuka au kwenda mahali pasipojulikana kwa kubahatisha. Mtume kwa msaada na mwongozo wa Allah, alichukua hatua za maandalizi zilizohitajika kwa safari hiyo.

Funzo hapa si kulinganisha moja kwa moja uhamiaji wa leo na Hijra ya Mtume, bali kujifunza kanuni ya kuwa na sababu, maandalizi na mpango kabla ya kuchukua hatua kubwa.

Leo baadhi ya vijana wanazamia nchi za watu. Wengine huondoka bila kujua watakachofanya wakifika huko. Wanaweza kuingia kwenye mazingira ya hatari, kudhulumiwa kazini, kupoteza fedha, kukosa nyaraka sahihi au kujikuta wakifanya mambo ambayo hawakuyapanga kabisa.

Uislamu unamtaka mtu kuchukua sababu na kufanya jitihada huku akimtegemea Allah. Kwa hiyo, kijana anayetaka kuhama anatakiwa kwanza kutafuta taarifa sahihi, kujifunza, kupanga, kutafuta njia halali ya kwenda na kuhakikisha anajua anachokwenda kufanya.

Lakini pia kijana anatakiwa kujiuliza swali muhimu: Je, kweli nimefanya kila nilichoweza hapa nchini kabla ya kuamua kuondoka? Huenda jibu likawa bado.

Huenda kijana wa Dar es Salaam akapata fursa kwenye kilimo, biashara, ufundi au teknolojia au katika kushirikiana na vijana wengine uliosoma nao au unaoishi nao mtaani. Vijana wa Kiislamu, msione aibu kuanza kidogo. Msidharau kazi halali kwa sababu si ya ofisini. Msidharau biashara kwa sababu inaanza na mtaji mdogo. Msidharau ufundi kwa sababu haukuhitaji miaka mingi ya elimu darasani.

Mafanikio bado yapo nchini. Tanzania lakini hata kama mtu ataamua kuhama, ahame kwa mpango thabiti, njia halali na uelewa wa mazingira ya anakokwenda. Asiende kwa msukumo wa mitandao ya kijamii au simulizi za watu wachache.






# Chapa binafsi: Jina lako lina thamani gani sokoni?

## JENGA chapa binafsi kupitia muonekano, tabia, unavyowasiliana na matumizi mitandao ya kijamii

Fikiria unatafuta mhasibu, fundi, mpiga picha au mshauri wa biashara. Unaambiwa majina ya watu wawili wenye elimu na uzoefu unaofanana. Mmoja unamfahamu kwa kazi zake nzuri, namna anavyowahudumia wateja na ushauri anaotoa mtandaoni. Mwingine humfahamu zaidi kwa jina.

Ni nani utakayemfikiria kwanza?

Katika biashara na ajira, watu hawachagui kwa kuangalia vyeti na bei pekee. Wanazingatia pia sifa, uaminifu na matarajio kuhusu huduma watakayopata. Hapo ndipo umuhimu wa kujenga brandi binafsi (personal brand) unapojitokeza.

Brandi binafsi ni taswira na sifa zinazojengeka akilini mwa watu kuhusu wewe. Unajulikana kwa nini? Una uwezo gani? Unawatendeaje wengine? Na mtu akikusikia ukitajwa, anakumbuka nini?

Kujenga brandi binafsi ni mchakato wa kimkakati wa kutambua thamani yako na kuiwasilisha kwa wengine. Lengo si kujitangaza tu, bali kuhakikisha watu wanaielewa kwa usahihi thamani unayotoa.

Hili si jambo la watu maarufu pekee. Mwalimu, daktari, mfanyabiashara, fundi, mwandishi wa habari au kijana anayetafuta ajira anaweza kujenga brandi binafsi.

Lakini mtu anaanzia wapi?

Njia mojawapo ni mfumo wa ABCD, unaoeleza kuzingatia mambo manne: mwonekano, tabia, mawasiliano na uwepo mtandaoni. Mfumo huu umeelezwa pia katika mwongozo wa taaluma unaounganisha mwonekano na uhalisia, tabia na mwenendo, mawasiliano na uaminifu, pamoja na uwepo kidijitali.

### A: Mwonekano (appearance)

Kabla hujazungumza, mara nyingi watu tayari wameanza kupata taswira fulani kukuhusu.

Mwonekano unahusisha mavazi, usafi, mpangilio na namna unavyojionesha katika mazingira ya kazi. Kwa mfanyabiashara, unaweza pia kujumuisha namna bidhaa zinavyopangwa, nyaraka zinavyowasilishwa na sehemu ya biashara inavyoonekana.

Haimaanishi kuvaa nguo za gharama kubwa au kuiga maisha ya watu wenye fedha. Fundi mwenye mavazi yanayofaa kazi yake na vifaa vilivyopangwa vizuri anaweza kutoa taswira ya kitaalamu kuliko mtu mwenye suti ya bei kubwa lakini kazi zake hazina mpangilio.

Mwonekano mzuri unatakiwa kuendana na kazi na watu unaowahudumia. Hata hivyo, mwonekano ni mlango tu. Hauwezi kufidia ukosefu wa ujuzi au huduma mbovu. Jiulize: Mteja anaponiona au anapofika katika eneo langu la kazi, anapata taswira inayolingana na huduma ninayoahidi?

### B: Tabia (Behavior)

Huu ndio mtihani mkubwa wa brandi binafsi.

Unaweza kuwa na picha nzuri, wasifu uliopangwa vizuri na maneno yenye kuvutia. Lakini tabia zako ndizo zitakazothibitisha kama watu wanapaswa kukuamini.

Unatimiza ahadi? Unafika kwa wakati? Unawaheshimu wateja? Unakubali makosa? Unatunzaje taarifa za watu unaowahudumia? Na mteja anapolalamika, unamsikiliza au unamshambulia? Unatendeaje wafanyakazi wako? Watu wanakukumbukaje katika mawasiliano na mahusiano yao nawe?

Matangazo yanaweza kufanya watu wakujaribu mara ya kwanza. Tabia yako inaweza kuwafanya warudi au waondoke kabisa.

### C: Mawasiliano (Communication)

Unaweza kuwa na ujuzi mkubwa lakini watu wasielewe unafanya nini, unamsaidia nani na kwa nini wakuchague. Hapa ndipo mawasiliano yanapokuwa sehemu ya brandi yako.

Jifunze kueleza thamani unayotoa kwa lugha rahisi. Mawasiliano yanajumuisha pia kusikiliza, kuuliza maswali, kuandika ujumbe unaoeleweka, kujibu maombi kwa wakati na kuwasilisha kazi kwa weledi.

Usitumie lugha ngumu kuthibitisha kwamba una elimu. Mtaalamu anayeeleza jambo gumu kwa namna ambayo mteja anaelewa anaonesha thamani ya maarifa yake.

Hata hivyo, kuwasiliana vizuri si kujisifu. Unaweza kujenga uaminifu kwa kueleza matatizo uliyotatua, kuonesha mifano ya kazi zako na kuwa mkweli kuhusu mambo yaliyo nje ya utaalamu wako.

### D: Uwepo mtandaoni (Digital Presence)

Zamani, mtu angeweza kutegemea zaidi watu waliomfahamu ana kwa ana. Leo, mteja au mwajiri anaweza kuanza kukuchunguza kupitia simu kabla hata hajakupigia. Atakuta nini akitafuta jina lako?

Wasifu wako wa LinkedIn, ukurasa wa Facebook, Instagram, tovuti, makala ulizoandika, kazi ulizochapisha na hata maoni unayotoa kwenye mijadala vinachangia taswira inayojengeka kukuhusu. Uwepo wa kitaalamu mtandaoni hujengwa kupitia maudhui, wasifu, mwingiliano na namna mtu anavyoonesha uzoefu na uwezo wake.

Pia chunguza unachoweka mtandaoni. Je, taarifa zako ni sahihi? Unatumia lugha gani unapokosoa wengine? Je, picha na maoni yako vinapingana na maadili unayodai kuyasimamia?

Na usichanganye wingi wa wafuasi na mafanikio ya biashara. Kilicho muhimu ni kuwafikia watu sahihi na kuwapa sababu ya kukuamini.

### Mambo manne, taswira moja

Mwonekano, tabia, mawasiliano na uwepo mtandaoni hayapaswi kuwa mambo manne yanayopingana. Ukitangaza uaminifu mtandaoni, uonekane katika huduma zako. Ukiahidi ubora katika mawasiliano yako, uthibitishwe na matokeo ya kazi. Ukijionesha kuwa mtaalamu, hakikisha unaendelea kujifunza.

Uhalisia, uthabiti na upekee vinaunganisha mambo hayo. Usiige taswira ya mtu mwingine kiasi cha kupoteza kile kinachokutofautisha. Brandi binafsi si kutengeneza picha nzuri ya mtu ambaye haupo. Ni kuifanya thamani yako halisi ionekane, ieleweke na ithibitishwe.

# Ukosefu wa uaminifu katika utawala wa Waqf Tanzania: Tatizo liko wapi?



## SEHEMU YA 2

**WIKI iliyopita, tulijadili tatizo la ukosefu wa uaminifu katika usimamizi wa mali za wakfu nchini Tanzania.**

**Tulieleza kuwa wakfu ni nyenzo muhimu ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika Uislamu, lakini uwezo wake wa kuvutia wafadhili na kuhudumia jamii unaweza kudhoofishwa na mashaka kuhusu usimamizi wake.**

**Tulibainisha mambo manne yanayoweza kuchochea mashaka hayo: ukosefu wa uwazi kuhusu mali na mapato yake; kutelekezwa kwa nyumba, viwanja na mali nyingine za wakfu; matumizi ya mapato yasiyoonesha wazi manufaa kwa walengwa; na kuingiliwa kwa usimamizi na maslahi ya makundi badala ya kuzingatia utaalamu.**

**Tulieleza pia athari zinazoweza kujitokeza: wafadhili kusita kuweka mali zao wakfu, miradi ya kudumu ya kijamii kukosa rasilimali, baadhi ya watu kupendelea miradi binafsi na mali za wakfu kuwa katika hatari ya kupotea.**

**Ikiwa tatizo ni uaminifu, suluhisho haliwezi kuwa kuwataka Waislamu watoe mali zaidi bila kuboresha usimamizi.**

**Swali la wiki hii ni: Tufanye nini kurejesha imani ya wafadhili, kulinda mali zilizopo na kuifanya wakfu iwe chanzo endelevu cha maendeleo? Tutajadili hatua nne zinazoweza kutusaidia kufikia lengo hilo.**

Upi uwe muelekeo mpya kuelekea ujenzi mpya wa uaminifu?

Ili kurejesha imani na kuifanya Waqf iwe chanzo chenye nguvu tena nchini Tanzania, mabadiliko ya mafanikio lazima yafanywe: kwenye maeneo manne (4)

### *Mosi,* Kuweka mifumo ya kisasa ya uhasibu (Digitalization & Auditing)

Taasisi zinazosimamia Waqf lazima zitenge fursa za kuandaa taarifa za kifedha (Financial Reports) kila mwaka na kuzifanyia ukaguzi wa nje na makampuni yanayotambulika kitaalamu. Hizi taarifa lazima ziweze kupatikana kwa umma (kwenye tovuti) ili kila Mtanzania aoneje fedha za Waqf zinatumiwaje.

### *Pili,* kuondoa siasa na kuweka wataalamu

Bodi za wafadhili na watendaji wa Waqf lazima ziweze kutengwa kabisa na siasa za vikundi. Wahitimu wa vyuo vikuu wanaofanya masomo ya uhasibu, uchumi, usimamizi wa mali (asset management), na sheria ndio wapaswao kuwa katika vikao vya kusimamia mali hizi.

Hata hivyo, usomi hautoshi peke yake, lazima wawe watu ambao ni waadilifu, wenye moyo wa kujitolea kwa ajili ya dini na wenye weledi wa hali ya juu.

### *Tatu,* Kuiraghibisha mali za waqfu kutoka "Waqf ya matumizi" kwenda "Waqf ya uzalishaji" (Productive Waqf)

Ili kuondoa shaka za wanajamii, mapato ya mali za Waqf yanapaswa kuwekwa kwenye miradi inayoonekana. Kwa mfano, badala ya kuacha kiwanja kitupu, kiwanja hicho kinaweza kujengwa maduka ya kisasa, na fedha za kodi za maduka hayo zikiahidiwa moja kwa moja kwa kusaidia wanafunzi masikini katika vyuo vikuu. Matokeo yanayonekana hujenga imani.

### *Nne,* Kuibuka kwa "Waqf ya Fedha" (Cash Waqf)

Kwa sababu watu wengi hawatoi ardhi kwa sababu ya ukosefu wa dhamiri katika taasisi kubwa, suluhisho la kisasa ni Waqf ya fedha. Hapa, wafadhili wanachangia fedha, hata kidogo kama shilingi 10,000) ambazo hushirikishwa katika mradi maalum (kama vile kununua mashine za hospitali).

Miradi hii inayoongozwa na wataalamu huru, yenye uwazi kamili, inaweza kuwa njia ya kuwavuta Waislamu wa kisasa wa Tanzania kurudi kwenye fursa hii ya Sadaqatul Jariyah.

### Hitimisho

Ukosefu wa dhamiri (Trust Deficit) sio tatizo la dini ya Uislamu, bali ni tatizo la binadamu na mifumo duni ya utawala.

Ikiwa tutafungua mlango wa uwazi, tutaweka wataalamu wenye uwezo, na tutaonyesha mapato ya Waqf, wazi, ni hatua kubwa. Waqf ni mali ya Mola na haina haki ya kutumika kama chombo cha kujigambizia, bali ni tiba ya matatizo ya kijamii na kiuchumi ya Waislamu nchini Tanzania.

NA Mahmoud Nyamguma

# Watoto Gaza majanga kila mahali, mwandishi mpalestina akamatwa

## Vita Gaza vimewarudisha watoto zaidi ya 280,000 madarasani katika mazingira ya mahema, magofu na uhaba wa vifaa, huku maelfu ya waliojeruhiwa wakikosa mahitaji muhimu.

Zaidi ya watoto 280,000 katika Ukanda wa Gaza wamerejea masomoni kwenye mahema na madarasa yaliyoharibiwa na vita, huku viti zaidi ya 900 vya magurudumu vilivyotolewa kusaidia watoto waliojeruhiwa vikiendelea kukwama nchini Jordan.

Kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi wa Palestina (UNRWA), watoto hao walianza mwaka mpya wa masomo Jumamosi, Septemba 19, 2026, katika mazingira yenye uhaba mkubwa wa vifaa.

Katika shule moja ya Nuseirat, watoto huketi kwenye blanketi sakafuni kutokana na ukosefu wa madawati. Mkuu wa Programu za Elimu wa UNRWA, Tawfiq Al-Hourani, amesema asilimia 95 ya shule 182 zilizokuwa na vifaa kamili miaka mitatu iliyopita zimepotea.

Wakati huohuo, uchunguzi wa ABC News umebaini kuwa viti zaidi ya 900 vilivyotolewa na mashirika mawili ya Australia vimekwama katika maghala nchini Jordan tangu mwaka 2025.

Shirika la Misaada la Hashemite la Jordan (JHCO) linasema mamlaka ya Israel inayoratibu misaada Gaza (COGAT) ilizuia shehena hizo kuingia, lakini Israel imekanusha kukataa ombi hilo.

Kwa mujibu wa UNICEF, watoto 45,000 wamejeruhiwa Gaza, wakiwamo zaidi ya 11,000 wenye majeraha yanayoweza kubadili maisha yao.

Katika tukio jingine, mamlaka za Israel zinamshikilia mwandishi Mpalestina mwenye uraia wa Marekani, Naqaa Hamed, aliyekamatwa Septemba 15 katika kituo cha ukaguzi cha Tuqu, karibu na Bethlehem, Ukingo wa Magharibi.

Kamati ya Kulinda Waandishi wa Habari (CPJ) imesema Hamed alikamatwa akirejea kutoka kazini, huku wapiga picha wawili aliokuwa nao wakiachiwa.

***Vyanzo: AP, ABC News, UNICEF, UNRWA, CPJ na Arab News.***



NA Mahmoud Nyamguma

# Abbas kuhutubia UN kwa video; EU yashinikiza Marekani impe viza

Rais wa Palestina, Mahmoud Abbas, anatarajiwa kuhutubia Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kwa video Alhamisi, Septemba 24, 2026, huku Umoja wa Ulaya (EU) ukiitaka Marekani kufikiria upya uamuzi wake wa kumnyima viza ya kuhudhuria mkutano huo jijini New York.

Baraza Kuu la UN liliidhinisha Septemba 17 Abbas kuwasilisha hotuba iliyorekodiwa mapema, baada ya Marekani kuendeleza zuio la viza kwa viongozi wa Palestina kwa mwaka wa pili mfululizo.

Azimio hilo lilipitishwa kwa kura 152 za ndiyo, tatu za hapana na nne zilizojizuia. Marekani, Israel na Paraguay zilipiga kura za kupinga.

Katika taarifa ya Septemba 19, Msemaji wa Sera za Kigeni wa EU, Anouar El Anouni, amesema umoja huo unasikitishwa na kuendelea kwa zuio hilo, ukisisitiza kuwa Marekani inapaswa kuzingatia wajibu wake kama nchi mwenyeji wa makao makuu ya UN.

Katibu Mkuu wa UN, António Guterres, pia ameonyesha kusikitishwa na hatua hiyo, akieleza wasiwasi kuhusu athari zake kwa uwezo wa Palestina kushiriki kikamilifu katika shughuli za umoja huo.

Marekani imetetea uamuzi wake, ikituhumu Mamlaka ya Palestina kushindwa kutekeleza ahadi za amani na kuendeleza hatua dhidi ya Israel katika mahakama za kimataifa. Palestina imepinga vikwazo hivyo.

Balozi wa Palestina katika UN, Riyad Mansour, amezishukuru nchi zilizounga mkono azimio hilo na kulaani uamuzi wa Marekani, akisema unawanyima viongozi wa Palestina haki ya kushiriki mkutano huo ana kwa ana.

Azimio la UN pia linawaruhusu wawakilishi wa Palestina kushiriki kwa video katika baadhi ya mikutano mingine ya ngazi ya juu ya kikao cha 81. Vyanzo: Anadolu Agency, Septemba 17 na 19, 2026; UN na Reuters.



NA Mahmoud Nyamguma



# Nigeria yakosa nafasi za ziada Hija

Saudi Arabia imekataa ombi la Nigeria la kuongeza idadi ya mahujaji kwa ajili ya Hija ya mwaka 2027, licha ya kuongezeka kwa Waislamu wanaotaka kutekeleza ibada hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa ya Septemba 17, 2026, ya Tume ya Taifa ya Hija ya Nigeria (NAHCON), nchi hiyo itaendelea kuwa na nafasi 50,000, zikiwamo 35,000 kwa mahujaji wa serikali na 15,000 kwa waendeshaji binafsi wenye leseni.

Mamlaka za Saudi Arabia zimesema zimekataa ombi hilo kutokana na ukomo wa uwezo wa kuhudumia mahujaji, changamoto za miundombinu katika maeneo matakatifu na utaratibu wa mgao wa kila nchi.

Mwenyekiti wa NAHCON, Ismail Abba Yusuf, amesema anatambua masikitiko ya Waislamu waliotarajia kupata nafasi zaidi, lakini tume yake inaheshimu uamuzi huo.

Chanzo: NAHCON na Muslim News Nigeria

## Saudi Arabia kusaidia mayatima 2,200 Gaza, Kosovo

**Saudi Arabia imesaini makubaliano mawili ya kutoa msaada kwa mayatima 2,200 katika Ukanda wa Gaza na Kosovo, yakilenga kupunguza changamoto za maisha na kuboresha ustawi wa watoto waliopoteza wazazi wao.**

**Kwa mujibu wa Shirika la Habari la Saudi Arabia (SPA), kupitia kituo chake cha misaada cha King Salman (KSrelief), nchi hiyo itawasaidia mayatima 1,500 wa Gaza kwa kushirikiana na Kituo cha Utamaduni na Urithi cha Saudi Arabia. Nchini Kosovo, KSrelief imesaini makubaliano na Jumuiya ya Kiislamu kusaidia mayatima 700 katika maeneo 29.**

**Mpango huo utatoa dola 100 kila mwezi kwa kila mtoto, pamoja na mavazi, mabegi, vifaa vya shule, midoli na shughuli za burudani na huduma nyingine za msingi.**

**Makubaliano yote mawili yametiwa saini Riyadh na Naibu Msimamizi Mkuu wa KSrelief anayeshughulikia Operesheni na Programu, Ahmed Al-Baiz.**

**Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2015, KSrelief imetekeleza miradi 4,463 yenye thamani ya karibu dola bilioni 8.6 katika nchi 113, Yemen ikiwa ni mfaidika mkuu (misaada ya thamani ya dola bilioni 4.8) ikifuatiwa na Syria, Palestina na Somalia.**

NA Mahmoud Nyamguma

# Mkurugenzi WFP asimulia mateso ya wasudan: njaa, vita na uhaba wa maji



Wanawake walisimama kwenye foleni wakisubiri maji, lakini ilipofika saa sita mchana, tanki likakauka. Walilazimika kurejea nyumbani na madumu matupu, wakiwa wamekata tamaa.

Hii ni moja ya simulizi ya mateso aliyoshuhudia Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Carl Skau, katika ziara yake ya siku nane nchini Sudan.

Katika mkutano na waandishi wa habari, Skau alisimulia kukutana na aliyekuwa mwanafunzi wa chuo kikuu, sasa akiishi kwenye kibanda cha wakimbizi. Alikuwa amepoteza wanafamilia, mama yake akiwa na msongo wa mawazo na baba yake mgonjwa. Alitamani kufanya kazi, lakini hakukuwa na fursa.

Huko Tawila, Darfur, karibu wakimbizi milioni moja wanaishi katika makazi ya muda. Wengi ni wanawake waliopoteza waume na watoto wao wa kiume kutokana na vita. WFP inawapatia chakula watu 950,000 kila mwezi, lakini mgao huo unatosha wiki mbili pekee. Wanawake wanahangaika kuufanya udumu hadi mgao unaofuata.

Katika mji wa El Fasher, Skau alikuta nyumba zilizotobolewa kwa risasi, magari yaliyoungua na mitaa iliyotelekezwa. Mji uliokuwa na wakazi milioni moja umebakiwa na makumi machache ya maelfu.


Baadhi ya familia zilizorejea zimekuta nyumba zao zimeteketea na kulazimika kutafuta hifadhi katika nyumba tupu. WFP inawafikia takriban watu 20,000 kwa chakula cha kuokoa maisha.

Sudan sasa inakabiliwa na janga kubwa zaidi la njaa na watu kuyakimbia makazi duniani. Watu milioni 20 wanakabiliwa na njaa kali, huku milioni 14 wakiwa wameyakimbia makazi yao. Skau ameonya kuwa uhaba wa fedha unaweza kulazimisha WFP kupunguza misaada zaidi katika wiki zijazo. Huko Darfur, ukame unatishia kilimo na mifugo, huku chakula cha msaada nacho kikihatarishwa.

Kwa familia zilizopoteza kila kitu, kupungua kwa msaada kunamaanisha kuendelea kuishi katika hali ya kutokuwa na uhakika wa kupata mlo unaofuata.

Na Said Rajab
0783 650 803

# Milango muhimu ya bahari na hatma ya uchumi wa dunia




## SEHEMU YA 1

**Ni ukweli usiopingika kwamba yeyote anayezidhibiti njia na milango ya bahari ana ushawishi mkubwa katika uchumi wa dunia. Swali la msingi la kujiuliza ni je, nani anayeshikilia funguo za njia hizi za bahari?**
**Milango bahari si njia za majini pekee; ni nguzo muhimu ya biashara ya kimataifa, inayowezesha usafirishaji wa bidhaa, mafuta, gesi na nishati kutoka sehemu moja ya dunia kwenda nyingine.**

Miongoni mwa njia muhimu zaidi za bahari ni Mlango–Bahari wa Hormuz, Bab al–Mandab na mfereji wa Suez. Usalama na utulivu wa maeneo hayo una athari za moja kwa moja kwa uchumi wa dunia, hususan katika bei za nishati na mwenendo wa biashara ya kimataifa.

Kutokana na uwepo wake wa kijeshi na ushirikiano wake na nchi za Mashariki ya Kati, Marekani ina ushawishi mkubwa katika masuala ya usalama wa milango hii ya bahari.

Marekani haihitaji kuufunga Mlango–Bahari wa Hormuz, kwa sababu hatua hiyo ingeathiri uchumi wa dunia, ukiwamo uchumi wa Marekani yenyewe. Kinachohitajika zaidi ni kuwa na uwezo wa kushawishi usalama, utulivu na uhuru wa urambazaji – lengo ambalo Marekani inalifuatilia kwa karibu na kulitumia kama turufu katika mazungumzo yake na Iran pamoja na wapinzani wake wengine.

Suala hili haliihusu Iran na Marekani pekee, bali linaweza pia kuathiri China na Ulaya. China inategemea mtiririko thabiti wa nishati na biashara, huku Ulaya ikiathiriwa moja kwa moja na mabadiliko ya bei za mafuta na gesi, pamoja na gharama za usafirishaji.

Hivyo, usumbufu wowote katika Mlango–Bahari wa Hormuz unaweza kusambaa na kugeuka kuwa mgogoro mkubwa wa kiuchumi, unaovuka mipaka ya eneo la Ghuba ya Uajemi.

Mwelekeo unaowezekana ni kurejea kwa hali ya kawaida ya urambazaji katika Mlango–Bahari wa Hormuz, lakini ndani ya mfumo wa makubaliano mapana ya kikanda – ambapo Marekani inaweza kuwa na jukumu muhimu katika kuyawezesha.

Tatizo lililopo ni kwamba dunia inataka Mlango–Bahari wa Hormuz ubaki wazi kwa wote, huku Marekani ikisisitiza kuwa masharti yake ya kiusalama kuhusu matumizi ya mlango huo yazingatiwe.

Vita halisi havihusu Mlango–Bahari pekee, bali pia vinawahusu wanaosimamia usalama wake na wale wenye uwezo wa kudhibiti njia zinazotumika katika usafirishaji wa biashara ya kimataifa.

***Tukutane wiki ijayo katika sehemu ya mwisho ya makala hii, Insha Allah***

ربيع ثان

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
0789 201383

# Kongole Saudia kwa mradi wa kilimo cha tende nchini

Tanzania na Saudi Arabia zimeanza kutekeleza mradi wenye thamani ya zaidi ya Sh bilioni mbili kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha tende katika maeneo yenye ukame, hususan mkoani Dodoma.

Utafiti wa kitaifa wa kilimo uliofanywa mwaka 2025 umeonesha kuwa zao la tende lina uwezo wa kustahimili mazingira ya ukanda huo, hivyo kutoa fursa kwa wakulima kuongeza wigo wa mazao yanayoweza kulimwa katika maeneo yenye ukame.

Akizungumza katika hafla ya utiaji saini mkataba wa mradi huo iliyofanyika Septemba 15, 2026 jijini Dodoma, Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde aliitaka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kutumia miche 250 ya tende iliyokabidhiwa kuzalisha miche zaidi ili kuwawezesha wakulima wa Hombolo kuanza kunufaika na zao hilo.

Naye Balozi wa Saudi Arabia nchini, Yahya Okeish, amesema nchi hiyo itaendelea kushirikiana na Tanzania kupitia wataalamu wake katika kuanzisha na kuendeleza kilimo cha tende nchini.

Hivyo, ni wazi kuwa mradi huo utaleta manufaa makubwa kwa nchi na wakulima kwa ujumla, kwani unatarajiwa kuongeza tija na kipato cha wakulima, huku ukifungua fursa mpya za ajira na biashara katika mnyororo wa thamani wa zao la tende.

Sisi, Gazeti la Imaan, tunaipongeza Saudi Arabia kwa hatua hii muhimu, inayofungua ukurasa mpya wa ushirikiano katika sekta ya kilimo.

Katika Uislamu, matumizi ya ardhi kwa ajili ya uzalishaji na kutafuta riziki halali yamepewa umuhimu mkubwa. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: "Yeye ndiye aliyeifanya ardhi iwe rahisi kwenu; basi tembeeni katika pande zake na kuleni katika riziki yake..." [Qur'an, 67:15].

Aya inatukumbusha wajibu wa kutumia ardhi na rasilimali tulizopewa kwa tija na kwa manufaa ya jamii. Kwa msingi huo, miche 250 iliyokabidhiwa kwa TARI inapaswa kuwa mwanzo wa uzalishaji wa miche mingine kwa wingi, hatua itakayosaidia kupanua kilimo cha tende nchini, kuchochea uchumi wa maeneo husika na kukuza uchumi wa taifa kwa ujumla.

Kwa upande mwingine, ni muhimu kuhakikisha wataalamu wetu wanajengewa uwezo ili kuendeleza maarifa na teknolojia za uzalishaji wa zao hili, na kuhakikisha manufaa yake yanaendelea kuonekana hata baada ya kukamilika kwa hatua za awali za mradi.

Kama alivyosema Balozi Okeish, kuwa Saudi Arabia itaendelea kushirikiana na Tanzania katika kuendeleza kilimo cha tende nchini. Hivyo, ni jukumu la wadau wote kuhakikisha fursa hiyo inatumika ipasavyo kwa kuwekeza katika uzalishaji wa miche na kuimarisha sekta ya uchakataji ili kuongeza thamani ya zao hilo.





SHEIKH
Seif Ruga
0712 690 811

# Hukumu za kifiqhi kuhusu muamala wa mudharaba



**Neno mudharaba, kwa lugha ya Kiarabu limetokana na maana ya “kupiga katika ardhi”, yaani kusafiri. Maana hiyo inahusishwa na safari za kutafuta riziki na kufanya biashara, kama Allah Mtukufu anavyosema: “…na wengine wanasafiri katika ardhi wakitafuta fadhila za Allah…” [Qur’an, 73:20].**

# Hukumu za kifiqhi kuhusu muamala wa mudharaba

Neno mudharaba, kwa lugha ya Kiarabu limetokana na maana ya "kupiga katika ardhi", yaani kusafiri. Maana hiyo inahusishwa na safari za kutafuta riziki na kufanya biashara, kama Allah Mtukufu anavyosema: "...na wengine wanasafiri katika ardhi wakitafuta fadhila za Allah..." [Qur'an, 73:20].

Katika lugha ya watu wa Madina, mudharaba pia huitwa qiradh, neno linalomaanisha "kukata". Jina hilo linarejelea kitendo cha mwenye mali kutenga sehemu ya mali yake na kumpa mtu mwingine ili aisimamie na kuiendesha kwa shughuli za biashara.

Katika muktadha wa sharia ya Kiislamu, mudharaba ni mkataba kati ya pande mbili. Upande mmoja hutoa mtaji, huku upande mwingine ukitoa nguvu, ujuzi na juhudi za kuendesha biashara. Faida inayopatikana hugawanywa kwa mujibu wa makubaliano yaliyowekwa.

Maana yake ni kwamba mwenye mali humpa mfanyakazi fedha ili afanye biashara, na faida inayopatikana hugawanywa kwa mujibu wa makubaliano yao.

Ni sharti kubainisha wazi sehemu au asilimia ya mfanyakazi katika faida, na si katika mtaji, kwa mfano nusu, theluthi au kiwango kingine cha asilimia kinachojulikana.

Ikiwa faida haikupatikana, mwenye mali atabaki na mali yake, ambayo ndiyo msingi wa biashara, huku mfanyakazi akiwa amepoteza nguvu, muda na jasho lake. Hii ni kwa sababu ushirika wao umejengwa katika faida ya biashara, na si katika msingi wa mali.

Iwapo hasara itapatikana, itamhusu mwenye mali pekee na si mfanyakazi (mzalishaji). Hasara ya mfanyakazi ni kupotea bure kwa juhudi na nguvu zake. Kubainisha kiwango cha mfanyakazi katika faida hufanywa kwa makubaliano. Mwenye mali, kwa upande wake, anastahiki sehemu yake kwa msingi wa mali aliyowekeza, si kwa sharti.

Ibn Al–Mundhir amesema kuwa wanazuoni wamekubaliana kwamba mfanyakazi anaweza kuweka sharti la kupata sehemu maalumu ya faida, yaani asilimia fulani, mradi kiwango hicho kijulikane wazi.

Muamala wa biashara ya mudharaba unaruhusiwa kwa makubaliano ya wanazuoni wote. Ushahidi wa makubaliano hayo ni kwamba, Mtume wa Allah (rehema na amani ziwe juu yake) aliukubali katika zama zake bila kuupinga.

Pia, mudharaba unaingia katika kauli ya Allah Mtukufu inayoruhusu biashara: "...na Mwenyezi Mungu amehalalisha biashara na ameharamisha riba..." [Qur'an, 2:275].

Kadhalika, unaingia katika biashara inayofanywa kwa ridhaa ya pande zote. Allah anasema: "Enyi mlioamini! Msiliane mali zenu kwa dhuluma, isipokuwa iwe biashara kwa kuridhiana baina yenu..." [Qur'an, 4:29].

## Muda na masharti ya mkataba

Miongoni mwa hukumu za mudharaba ni kwamba unaweza kuwekwa kwa muda maalumu au kufungwa kwa sharti fulani la baadaye, kwa kuwa ni aina ya ruhusa ya kufanya shughuli.

Mfanyakazi (mzalishaji) haruhusiwi kutumia mali ya mudharaba kwa manufaa binafsi, ikiwamo kugharamia maisha au matibabu yake, au kuitumia katika safari na shughuli nyingine za biashara bila makubaliano na mwenye mali.

Mfanyakazi ni kama mwajiriwa katika kazi anayoifanya, na kwa upande mwingine anakuwa mshirika pale faida inapopatikana, kwa kuwa hupata sehemu ya faida hiyo.

Hawezi kudai zaidi ya faida hiyo isipokuwa kwa sharti maalumu au kwa desturi inayokubalika, kwa kuzingatia kanuni isemayo: "Linalojulikana kwa desturi ni kama lililowekewa sharti."

Mfanyakazi hastahiki chochote katika faida mpaka mtaji ukamilike kwanza. Ikiwa mkataba wa mudharaba utaharibika au kubatilika, mfanyakazi hatopata faida, bali atalipwa ujira wa kawaida wa kazi yake.

Hii ni kwa sababu haki yake ya faida ilikuwa imefungwa kwa sharti, na sharti hilo huondoka pindi mkataba unapobatilika, kwa mujibu wa kanuni isemayo: "Asili ikiondoka, tawi nalo huondoka." Ama mwenye mali, faida yote hubaki kwake, kwa kuwa faida ni ongezeko la mali yake.

## Kuuza mali ya mudharaba

Mfanyakazi ana haki ya kuuza mali ya mudharaba kwa fedha taslimu, kwa kuwa lengo kuu la mkataba huo ni kufanya biashara na kupata faida. Hata hivyo, kwa kuwa mali hiyo ni amana, mfanyakazi haruhusiwi kuitumia au kuishughulikia kwa namna inayoweza kumdhuru mwenye mali bila kupata ruhusa yake.

Faida inayopatikana kati ya pande mbili hutumika kulinda mtaji, hivyo hairuhusiwi kugawanywa kabla ya mkataba kumalizika, isipokuwa kwa makubaliano ya pande zote.

Faida hiyo pia inaweza kutumika kufidia hasara inayoweza kujitokeza katika baadhi ya shughuli za biashara. Ikiwa faida itagawanywa mapema, basi hakutakuwa na akiba ya kufidia hasara inayoweza kutokea baadaye.

Katika hali ya mgogoro, kauli ya mfanyakazi kuhusu shughuli za biashara huzingatiwa – iwe alizifanya kwa ajili yake mwenyewe au kwa mujibu wa mkataba wa mudharaba, kwa kuwa amepewa dhamana ya kusimamia mali hiyo.

Hata hivyo, mfanyakazi atawajibika kufidia hasara endapo itatokana na matumizi mabaya ya mali au uzembe katika kuitunza. Lakini ikiwa hakufanya kosa wala kuwa mzembe, hatabeba dhamana ya hasara hiyo, kwa mujibu wa makubaliano ya wanazuoni.



ربيع ثان

**NASAHA ZA WIKI**

0787 503 085



NA YUSUFU AMINI

# Unahitaji kupendwa na Allah? Zingatia haya

**Mtu akisema, "Nampenda Allah," ilhali hamtii wala kumuabudu, huyo ni mwongo, kwa sababu upendo wa kweli kwa Allah hudhihirika katika kumtii, kumuabudu, kumtegemea Yeye pekee na kufuata mafundisho ya Mtume wake (Allah amshushie rehema na amani).**

**Kumpenda Allah hakupimwi kwa maneno tunayoyasema, bali kwa matendo yanayobadili mwenendo wetu hapa duniani na kutuelekeza kutafuta radhi za Allah na malipo mema Akhera.**

**Sasa hebu tuangalie mambo 10 yanayomuweka mja karibu na Allah na kumfanya apate mapenzi yake, kama alivyoeleza Imam Ibn Qayyim al–Jawziy (Allah amrehemu) katika kitabu chake kiitwacho "Madarij as–Salikin."**

### *Jambo la kwanza* ni kusoma Qur'an kwa tafakuri

Kusoma Qur'an kwa wingi na kwa mazingatio ni njia muhimu ya kumjua Allah na kuimarisha uhusiano wako na Yeye. Allah anasema: "Je, hawaizingatii Qur'an, au nyoyo zao zina kufuli?" [Qur'an, 47:24].

Muislamu anapoisoma Qur'an kwa moyo wa kutafakari, hujifunza kuhusu rehema, uwezo, hekima na ukuu wa Mola wake.

### *Pili,* kutekeleza ibada za Sunna

Baada ya kutekeleza ibada za faradhi, mja anapaswa kuongeza ibada za Sunna.

Katika Hadithil Qudsi iliyopokelewa na Imam Bukhari kutoka kwa Abu Huraira (Allah amridhie), Mtume (Allah amshushie rehema na amani) ametueleza kwamba, Allah Aliyetukuka anasema: "Mja wangu haachi kujikurubisha kwangu kwa ibada za ziada mpaka nimpende."

Ibada za Sunna ni sehemu muhimu ya maisha ya Muislamu, kwani humsaidia kuimarisha uhusiano wake na Allah, kupata mapenzi yake (Mahabbatullah), pamoja na ulinzi na mwongozo wake katika maisha.

### *Tatu,* kumdhukuru Allah kwa wingi

Dhikr ni chakula cha moyo. Mtu anapomtaja Allah mara kwa mara, moyo wake huendelea kuwa na uhusiano mzuri na Mola wake hata akiwa katika shughuli za kila siku. Allah anasema: "Enyi mlioamini! Mkumbukeni Allah kwa wingi wa kumkumbuka." [Qur'an, 33:41].

Pia Mtume ametufundisha kwamba mfano wa anayemtaja Allah na asiyemtaja ni kama mfano wa aliye hai na aliyekufa. Hivyo, ulimi unaomtaja Allah na moyo unaomkumbuka huimarisha mapenzi hayo.

### *Nne,* kutanguliza anayoyapenda Allah

Upendo wa kweli huonekana zaidi pale matakwa ya mtu yanapogongana na amri ya Allah. Mja anayempenda Allah huonesha utiifu kwake hata pale nafsi yake inapopendelea mambo mengine.

Allah anasema: "...ikiwa mnampenda Mwenyezi Mungu, basi nifuateni mimi (Muhammad); Allah atawapenda na atawasamehe madhambi yenu." [Qur'an, 3:31].

### *Tano,* kutafakari majina na sifa za Allah

Kumjua Allah ni msingi wa kumpenda. Muislamu anapotafakari kwamba Allah ni mwenye kurehemu, mwenye kusamehe, mwenye hekima na mwenye kuruzuku, moyo wake hujaa matumaini na mapenzi kwake.

Kwa hiyo, kujifunza majina na sifa za Allah si elimu ya darasani pekee, bali ni njia ya kuujenga na kuutakasa moyo.

### *Sita,* kutafakari neema za Allah

Mwanadamu amezungukwa na neema nyingi ambazo wakati mwingine huzichukulia kuwa za kawaida. Uhai, afya, akili, riziki, usalama na uwezo wa kutubu ni miongoni mwa neema hizo.

Qur'an inasema: "Na mkihesabu neema za Allah, hamtoweza kuzidhibiti." [Qur'an, 16:18]. Mtu anapopewa neema nyingi, anapaswa kuongeza shukrani na kuimarisha mapenzi yake kwa Allah.

### *Saba,* kumnyenyekea Allah

Moyo unaompenda Allah hujinyenyekeza kwake kupitia sala, toba na dua, hasa wakati wa matatizo. Muislamu anapokumbwa na shida, hakati tamaa; badala yake humgeukia Allah kwa unyenyekevu na matumaini.

### *Nane,* kusali sala za usiku

Usiku ni wakati wa utulivu unaompa mtu nafasi ya kutafakari na kujitathmini. Kwa sababu hiyo, kusali Tahajjud, kusoma Qur'an na kuomba dua wakati huo ni miongoni mwa njia zinazosaidia kuimarisha uhusiano na Allah.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) ameeleza kwamba katika theluthi ya mwisho ya usiku, Allah huteremka katika mbingu ya dunia na kusema: "Nani ananiomba nimuitikie? Nani ananiomba jambo nimpe? Nani ananiomba msamaha nimsamehe?" [Bukhari na Muslim].

### *Tisa,* kushikamana na watu wema

Marafiki wana nafasi kubwa katika maisha ya mtu. Kusuhubiana na watu wanaomkumbuka Allah, wanaopenda ibada na wanaoepuka maovu humsaidia Muislamu kuimarisha imani yake.

Mtume amesema kuwa mtu hufuata dini ya rafiki yake wa karibu. Hivyo, kila mmoja anapaswa kuangalia ni nani anayemchagua kuwa rafiki yake.

### *Kumi,* kuepuka mambo yanayouharibu moyo

Upendo wa Allah unahitaji kulindwa na kutunzwa. Kutenda dhambi, kujishughulisha kupita kiasi na mambo ya dunia na kujiweka katika mazingira yanayokuweka mbali na ibada kunaweza kudhoofisha uhusiano wako na Allah.

Kwa hiyo, ikiwa unatamani kupendwa na Allah, tunza moyo wako kwa kuzidisha ibada na kujiepusha na mambo yanayoweza kukuweka mbali na Mola wako.



# ELIMU YA MAZISHI YA KIISLAMU

## Jinsi ya kuosha maiti kwa mujibu wa Sunna: Hatua kwa hatua

**SEHEMU YA 6**

**Katika makala iliyopita tulieleza kwamba kumuosha Muislamu aliyefariki ni Faradhi Kifayah na kwamba ni ibada inayopaswa kufanywa kwa heshima na uaminifu. Leo tutaangalia namna Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alivyotufundisha kuosha maiti.**

**Ni muhimu kufahamu kwamba lengo la kuosha maiti si kuusafisha mwili kwa namna ya kawaida, bali ni kutekeleza ibada kwa kufuata Sunna. Kwa hiyo, kila hatua inapaswa kufanywa kwa utulivu, staha na kumkumbuka Allah.**

### Hatua ya kwanza: Kuandaa mahali pa kuoshea

Mahali pa kuoshea maiti panapaswa kuwa safi, penye faragha, pasipo na msongamano wa watu na panapolinda heshima ya marehemu. Na wala si jambo la Sunna kuwaruhusu watu wengi kuingia kutazama zoezi la kuosha maiti. Wanaohitajika wawe wale wanaoshiriki moja kwa moja katika kuosha au kusaidia.

### Hatua ya pili: Kusitiri mwili wa marehemu

Sehemu za siri za marehemu lazima zisitiriwe tangu mwanzo wa kuosha mpaka mwisho wake. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amefundisha kuhifadhi heshima ya Muislamu akiwa hai na baada ya kufa. Hivyo, hakuna ruhusa ya kufunua mwili wote bila sababu ya lazima.

### Hatua ya tatu: Kuondoa najisi

Kabla ya kuanza kuosha mwili wote, huondolewa uchafu wowote uliotoka mwilini. Mwenye kuosha anatakiwa kutumia kitambaa au glovu ili asiguse sehemu za siri za marehemu moja kwa moja bila haja.

### Hatua ya nne: Kumtawadhisha

Wanazuoni wengi wameeleza kuwa ni Sunna kumtawadhisha maiti kama wudhu wa Swala. Hili hufanywa kwa kuoshwa uso wake, mikono, hupanguswa kichwa (kwa namna inayofaa) na kuoshwa miguu. Maji hayaingizwi kwa nguvu puani wala mdomoni, bali husafishwa kwa upole ili kuepusha madhara kwa mwili.

### Hatua ya tano: Kuosha kichwa na nywele

Baada ya wudhu, maiti huoshwa kichwa na nywele kwa maji yaliyochanganywa na mkunazi au sabuni nyingine inayofaa. Ikiwa marehemu ni mwanamke mwenye nywele ndefu, nywele zake huoshwa kwa upole na kusukwa katika mafundo matatu kama ilivyofanywa kwa binti wa Mtume (Allah amshushie rehema na amani).

### Hatua ya sita: Kuosha mwili

Maiti huanzia kuoshwa upande wa kulia, kwa kufuata Sunna ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani) aliyependa kuanza upande wa kulia katika mambo ya heshima. Baada ya hapo huoshwa upande wa kushoto. Kisha, hufuata mgongo na sehemu nyingine za mwili – na katika hatua zote hizi maiti husafishwa vizuri kwa upole, bila kutumia nguvu zinazoweza kuharibu mwili.

### Hatua ya saba: Kurudia kuosha

Asili ni kuosha mara tatu. Ikiwa mwili haujasafika vizuri, huongezwa mara tano au saba kwa idadi ya witri (isiyo na jozi), kulingana na haja. Hii inatokana na hadith ya Ummu 'Atwiyyah ambapo Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alisema: "Mwosheni mara tatu, au tano, au zaidi ya hapo mkiona inafaa." Hivyo, idadi si lengo lenyewe bali usafi wa mwili na kufuata Sunna ndio msingi.

### Hatua ya nane: Josho la mwisho

Katika josho la mwisho hupendekezwa kuwekwa kiasi cha kafuri. Kafuri hutoa harufu nzuri na pia husaidia kuufanya mwili ubaki katika hali nzuri kwa muda mfupi kabla ya kuzikwa.

### Hatua ya tisa: Kukausha mwili

Baada ya kumaliza kuosha, mwili hukaushwa kwa kitambaa safi ili kuondoa unyevunyevu kabla ya kuvikwa sanda. Hatua hii hurahisisha kumvika sanda na kuhifadhi usafi wa sanda.

### Hatua ya kumi: Kumpeleka kwa ajili ya kusanda

Baada ya kuoshwa, maiti hupelekwa mara moja kwa ajili ya kuvikwa sanda, bila kuchelewesha. Lengo ni kuendelea na taratibu za Janaza kwa haraka kama alivyoelekeza Mtume (Allah amshushie rehema na amani).

### Masuala muhimu ya Kifiqhi

Wanazuoni wameeleza kwamba ikiwa mwili umeungua sana, umeharibika kutokana na ajali na pengine kutokana na hali hizo kuoshwa kutasababisha kuharibika zaidi; basi huoshwa kwa namna inayowezekana. Ikiwa hata hilo haliwezekani, hukumu huhamia kwenye tayammum, kwa mujibu wa kauli ya wanazuoni wengi, kwa kuzingatia kanuni ya Sharia: "Mcheni Allah kadiri mnavyoweza." [Qur'an, 64: 16]. Hii inaonesha kwamba Sharia imejengwa juu ya urahisi, si uzito.

### Makosa yanayoonekana katika jamii

Baadhi ya makosa yanayojitokeza ni kutumia manukato au kemikali nyingi kupita kiasi; kuamini kuwa lazima kuwe na idadi maalumu ya watu wanaoosha maiti na kutumia maji ya moto sana au baridi sana bila sababu.

Makosa mengine ni kufanya mazungumzo yasiyo na adabu wakati wa kuosha; kupiga picha au kurekodi video; na kuchelewesha kuvika sanda baada ya kuosha. Makosa haya hayana msingi katika Sunna na yanapunguza heshima ya ibada hii.

### Hitimisho

Kuosha maiti ni ibada inayofundisha huruma, staha na udugu. Muislamu anapomuosha ndugu yake, anatambua kwamba wote wanaelekea mwisho mmoja. Leo yeye ndiye anayehudumia; kesho huenda akahitaji kuhudumiwa.

Ndiyo maana wanazuoni walikuwa wakiona kushiriki katika kuosha na kuzika maiti kuwa ni miongoni mwa ibada zinazolainisha moyo na kumkumbusha mwanadamu Akhera.

Na Said Rajab

0783 650 803

# Kujali ndugu kunavyodumisha mshikamano wa familia

## SEHEMU YA 1

**Kuwatendea wema ndugu na kuwaonesha ukarimu ni miongoni mwa matendo yenye thamani kubwa katika Uislamu. Hii ni kwa sababu ndugu ana haki mbili kwa ndugu yake: haki inayotokana na Uislamu na haki inayotokana na udugu wa kifamilia.**



Qur'an Tukufu inasisitiza kwa kiasi kikubwa umuhimu wa kuwaheshimu na kuwafanyia wema ndugu, pamoja na watu wengine wanaotuzunguka. Kufanya hivyo ni miongoni mwa matendo mema yanayomkaribisha mtu zaidi kwa Allah na kuchangia kujenga jamii yenye mshikamano.

Allah anasema: "Muabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote. Na wafanyieni wema wazazi wawili na jamaa na mayatima na masikini na jirani wa karibu na jirani wa mbali, na rafiki wa ubavuni na mpita njia..." ***[Qur'an, 4:36].***

Katika aya nyingine, Allah anasisitiza wajibu wa kuwapa ndugu haki zao: "Na mpe jamaa wa karibu haki yake, na masikini, na msafiri (aliyeharibikiwa), na wala usitumie ovyo kwa fujo." ***[Qur'an, 17:26].***

Aya hizi zinaeleza wazi kwamba kuwajali na kuwasaidia ndugu si suala la hiari linalotegemea mazingira au hali ya uhusiano pekee, bali ni sehemu ya maadili ambayo Uislamu unayahimiza. Kuwasaidia wakati wa shida, kuwafariji wanapopitia changamoto na kushirikiana nao katika nyakati za furaha ni miongoni mwa njia za kuimarisha uhusiano wa kifamilia.

Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) ameufanya uhusiano huu kuwa miongoni mwa alama za imani, akiuunganisha moja kwa moja na imani ya Muislamu. Mtume amesema: "Mwenye kumuamini Allah na Siku ya Mwisho, basi adumishe mafungamano yake ya kidugu." [Bukhari na Muslim].

Pia amesema: "Mwenye kudumisha udugu si yule anayelipa (mema anayofanyiwa), bali ni yule anayeunga udugu hata pale ndugu zake wanapomkata." [Bukhari].

Kwa msingi huo, kudumisha udugu hakumaanishi tu kurudishiana wema kwa wema. Udugu wa kweli hujitokeza kwa dhahiri zaidi pale familia inapokumbwa na misukosuko, migawanyiko na utengano.

Muumini anapaswa kuwa mstari wa mbele katika kutafuta suluhu, kuanzisha salamu, kuvumilia na kupuuza makosa madogo, huku akitarajia thawabu kutoka kwa Allah.

Mtume (rehema na amani zimshukie) ameeleza pia kuwa kudumisha uhusiano wa kifamilia ni miongoni mwa sababu zinazochangia kuongezeka kwa riziki na kurefushwa kwa maisha.

Mtume amesema: "Yeyote anayetaka riziki yake iongezwe na maisha yake yarefushwe, basi adumishe uhusiano wake wa kidugu." [Bukhari na Muslim].

Makosa, kutoelewana na kupitia nyakati ngumu ni sehemu ya maisha ya kifamilia. Hata hivyo, muumini wa kweli ameamrishwa kusamehe na kupuuza makosa, badala ya kuruhusu kosa la muda mfupi kuwa chanzo cha mgogoro wa kudumu au kutengana kwa muda mrefu.

Allah anasema katika Qur'an: "Na wala wasiape wale wenye fadhila miongoni mwenu na wenye wasaa wa mali kuwa hawatowapa (sadaka) jamaa wa karibu, na masikini, na Muhajirin katika njia ya Allah. Na wasamehe na waachilie mbali. Je, nyinyi hampendi Allah akusameheni? Na Allah ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu." ***[Qur'an, 24:22].***

Katika aya nyingine, Allah Ta'ala anasema: "Mema na maovu hayalingani. Pinga uovu kwa lilio jema zaidi. Hapo yule ambaye baina yako naye pana uadui atakuwa kama rafiki jamaa wa kukuonea uchungu." ***[Qur'an, 41:34].***

Aya hizi zinamuongoza Muislamu kujibu makosa anayotendewa kwa msamaha. Aidha, zinamkumbusha kwamba yeyote anayetarajia msamaha wa Allah, naye anapaswa kuwasamehe waja wake.

*Itaendelea wiki ijayo Insha Allah*

NA SAMRATH MSUYA
0789 201 383

SEHEMU YA 2

## Kabla ya kuoana, wafundishwe nini?

# Mnapotuandaa kwa harusi kuliko maisha ya ndoa ni tatizo

**WIKI iliyopita nilijadili tofauti kati ya maandalizi ya harusi na maandalizi ya ndoa. Harusi ni tukio; ndoa ni maisha yanayofuata baada yake. Sasa tujiulize: Kama tunakubaliana kwamba watu wanapaswa kuandaliwa kwa ndoa, wafundishwe nini? Sitaki hapa kufundisha namna ya kuishi kwenye ndoa. Ninapendekeza maeneo muhimu ya kuingizwa katika programu yenye mtaala kwa wanaume na wanawake wanaotarajia kuoana. Mafunzo hayo yasiwe hotuba ya saa moja siku chache kabla ya nikah.**

### *Mosi:* Fiqh ya ndoa iwe msingi

Mtarajiwa anapaswa kuelewa maana na madhumuni ya ndoa katika Uislamu, mkataba wa nikah, mahari, haki na wajibu wa wanandoa, masharti yanayoweza kuwekwa kwenye mkataba na mipaka ya Sharia.

Hata haki za faragha na mahusiano ya kimwili zina nafasi katika elimu hii. Tusiwaache vijana wajifunze mambo ya msingi kutoka kwa marafiki na mitandaoni pekee.

### *Pili:* Mawasiliano na utatuzi wa migogoro

Watu wawili wanaweza kuwa wema lakini wakashindwa kuishi pamoja kwa sababu hawajui kuwasiliana.

Wafundishwe kusikiliza, kueleza mahitaji, kutofautiana bila kutukanana, kuomba msamaha, kukubali makosa, kufanya maamuzi kwa mashauriano na kutatua matatizo kabla hayajageuka chuki. Tusisubiri ugomvi mkubwa ndipo watafute stadi hizi.

### *Tatu:* Fedha zizungumzwe kabla ya ndoa

Wanaotarajia kuoana wazungumzie kipato, madeni, matumizi, akiba, bajeti, wajibu wa kifedha, matarajio kuhusu kazi ya mke au mume na msaada kwa ndugu. Si lazima kila familia iwe na utaratibu unaofanana. Muhimu ni watu wawili kujua hali wanayoingia na kukubaliana namna ya kuisimamia.

Deni kubwa la mmoja lisije kuwa mshangao miezi sita baada ya harusi.

### *Nne:* Wazazi, wakwe na familia pana

Ndoa huunganisha familia mbili. Hivyo, mafunzo yajumuishe heshima kwa wazazi na wakwe pamoja na mipaka ya kuingilia maisha ya wanandoa. Wazungumzie kuishi na wazazi, kuwahudumia wanapozeeka, ziara za ndugu, msaada wa kifedha na kutunza siri za ndoa.

Migogoro kati ya mwenza na familia yake itashughulikiwaje? Mazungumzo haya yafanyike mapema.

### *Tano:* Malezi ya watoto

Je, mazungumzo kuhusu malezi yasubiri mtoto azaliwe? Wanaotarajia kuoana wajadili matarajio yao kuhusu kupata watoto, nidhamu, elimu, dini na mgawanyo wa majukumu ya kuwalea.

Tofauti kubwa za mitazamo zinaweza kuleta migogoro. Hata malezi ya mtoto wa mwenza kutoka ndoa iliyopita yanahitaji kuzungumziwa.

### *Sita:* Afya na mahusiano ya kimwili

Aibu isituzuie kutoa elimu sahihi kuhusu afya ya uzazi, usafi, mahusiano ya kimwili, ridhaa, mawasiliano na haki za kila upande. Watarajiwa waelezwe pia umuhimu wa uwazi kuhusu magonjwa sugu, matumizi ya dawa, uraibu na changamoto za afya ya akili zinazoweza kuathiri maisha ya familia.

Masuala haya yanahitaji elimu na ushauri unaofaa, si kuyaficha hadi baada ya ndoa.

### *Saba:* Tabia, hasira na historia ya mtu

Tunachunguza kazi, elimu na familia ya mtu, lakini je, tunachunguza namna anavyoshughulikia hasira? Mafunzo yawasaidie watarajiwa kutathmini tabia za kudhibiti, kutisha au kudhalilisha wengine, pamoja na athari za historia ya ukatili.

Hapa tunahitaji pia wataalamu wa saikolojia na ushauri nasaha, si sheikh pekee.

### *Nane:* Tamaduni na matarajio

Hata watu wa dini moja wanaweza kutoka familia zenye desturi tofauti. Mmoja anaona ni kawaida ndugu kuingia nyumbani wakati wowote; mwingine anathamini faragha. Mwingine ana matarajio tofauti kuhusu majukumu ya mke au mume.

Katika Tanzania yenye tamaduni nyingi, mafunzo yajenge uwezo wa kuzungumza, kuelewana na kuheshimu tofauti.

### *Tisa:* Sheria na nyaraka

Watarajiwa wanahitaji elimu ya msingi kuhusu usajili wa ndoa, nyaraka, mali, mirathi, watoto, wajibu wa kisheria na matokeo ya kuvunjika kwa ndoa. Ndoa ni mkataba pia. Masharti na masuala muhimu yazungumzwe kabla ya maisha ya pamoja kuanza, si wakati mgogoro umeshatokea.

### *Kumi:* Wapi pa kupata msaada?

Mafunzo yasiishie kwenye kauli, "Mkigombana, vumilianeni."

Wanandoa wajue namna ya kupata msaada wa wazee wenye busara, maimamu, washauri wa ndoa, wataalamu wa afya ya akili na huduma za upatanishi.

Qur'an inatambua nafasi ya waamuzi kutoka pande mbili mgogoro wa ndoa unapokuwa mkubwa. Msaada utafutwe mapema, si wakati mambo yameharibika sana.

Hapa ndipo natamani tufike: Badala ya mkungwi mmoja kufundisha kila kitu, sheikh kutoa mawaidha ya dakika 20 na familia kusema "mengine mtajifunza wenyewe," tuwe na programu inayowakutanisha wanazuoni, washauri wa ndoa na wataalamu wa fedha, afya na sheria, pamoja na wanandoa wenye uzoefu.

Hatuhitaji kuahidi ndoa zisizo na matatizo. Tunahitaji kuwawezesha watu wasiingie humo bila maarifa na zana za kukabiliana na changamoto.

Maandalizi mazuri ya ndoa hayazuii kila dhoruba; yanawapa wanaooana uwezo wa kuendesha jahazi dhoruba inapokuja.

Na Samrath Msuya
0789 201 383

# Mfanyakazi hafanyi vizuri? Jiulize maswali haya matatu

**KUNA mfanyakazi anayekawia kuwasilisha kazi, mwingine anarudia makosa yale yale, na mwingine anaonekana kupinga kila anachoelekezwa. Kiongozi anapochoshwa na hali hiyo, ni rahisi kufikia hitimisho: "Huyu mfanyakazi ni mvivu, mkaidi na hafai." Lakini kabla ya kumhukumu, kuna swali muhimu: Je, tumegundua chanzo halisi cha tatizo?**

**Mshauri wa uongozi na mtunzi wa vitabu, Christy Rutherford kutoka Marekani anapendekeza maswali matatu ya kuanzia: Je, mfanyakazi ana ujuzi unaohitajika? Je, mazingira yanamwezesha kufanya kazi? Na je, yuko tayari kuwajibika?**

**Maswali hayo yanaweza kumsaidia kiongozi kuacha kuongozwa na hasira na kuanza kutafuta suluhisho linalolingana na tatizo.**

## *Kwanza,* ana ujuzi unaohitajika?

Fikiria mfanyakazi ambaye ripoti zake zina makosa mengi na zinarudishwa kufanyiwa marekebisho, kiongozi anaweza kudhani hana bidii. Lakini je, amewahi kupatiwa mafunzo ya uandishi wa ripoti? Anaelewa viwango vinavyotakiwa? Amepewa mfano wa ripoti nzuri?

Somo hapa si kwamba kila anayeshindwa kazi hana uwezo wa kujifunza. Ni kwamba ukosefu wa ujuzi hauwezi kutatuliwa kwa lawama pekee.

Kama tatizo ni maarifa, suluhisho linaweza kuwa mafunzo, mwongozo, usimamizi wa karibu au kumpangia mfanyakazi majukumu yanayolingana zaidi na uwezo wake. Kumkaripia kila siku mtu ambaye hajui kufanya kazi fulani hakumfundishi kuifanya.

## *Pili,* mazingira yanamwezesha kufanya kazi?

Mfanyakazi anaweza kuwa na ujuzi mzuri lakini akashindwa kuutumia kikamilifu kutokana na mazingira yanayomzunguka.

Huenda amepewa kazi nyingi kuliko muda uliopo, hana vifaa, anapitia changamoto za kifamilia au amewekwa kwenye nafasi ambayo haitumii vizuri uwezo wake.

Rutherford anaeleza mfano wa mfanyakazi aliyekuwa akionekana kutofanya vizuri, lakini alipohamishiwa majukumu yaliyolingana na mambo aliyopenda na kupewa muda wa kujifunza, utendaji wake ulibadilika.

Wakati mwingine tatizo si mtu kutotaka kufanya kazi. Ni kwamba mfumo haumwezeshi kufanya kazi vizuri.

## *Tatu,* yuko tayari kuwajibika?

Hata hivyo, si kila tatizo la utendaji linasababishwa na ukosefu wa ujuzi au mazingira mabovu.

Kuna wakati mfanyakazi ana maarifa, nyenzo na msaada unaohitajika, lakini anaendelea kukataa kutekeleza majukumu, kuvunja taratibu au kuwatendea vibaya wenzake.

Hapo kiongozi anapaswa kuchunguza utayari wake wa kubadilika. Lakini hitimisho hilo lisifikiwe kutokana na kosa moja, tetesi au hisia binafsi. Linahitaji ushahidi wa mwenendo, mazungumzo ya wazi na nafasi ya mfanyakazi kueleza upande wake.

Rutherford anasisitiza kuwa kuendelea kuvumilia mwenendo unaodhuru kazi kuna gharama kwa timu nzima, hasa pale msaada na hatua za kurekebisha tatizo zinapokuwa hazijaleta mabadiliko.

Huruma haimaanishi kuacha kuwajibisha.

## Na kiongozi mwenyewe je?

Kabla ya kusema mfanyakazi ndiye tatizo, kiongozi anapaswa pia kujiuliza maswali magumu.

Je, nilieleza majukumu yake vizuri? Nilimpa vifaa vinavyohitajika? Ninamwelekeza au ninamkumbuka anapokosea tu? Je, mzigo wa kazi unawezekana? Nimejenga mazingira ambayo watu wanaweza kusema wanapokwama?

Maandiko kuhusu usimamizi wa wafanyakazi yanaonesha kuwa matatizo ya utendaji yanaweza pia kuhusishwa na mawasiliano duni kutoka kwa viongozi, ukosefu wa mafunzo, mzigo mkubwa wa kazi na kutokulingana kwa matarajio na majukumu halisi.

Mfanyakazi ana wajibu wake, lakini kiongozi naye ana wajibu wa kujenga mazingira yanayowezesha kazi kufanyika.

## Usimlalamikie pembeni, zungumza naye

Kuna tatizo pia la viongozi wanaomlalamikia mfanyakazi kwa wenzao badala ya kukaa naye na kumweleza wazi mwenendo unaohitaji kubadilika. Tatizo linaachwa likue hadi kiongozi anapoanza kufikiria kumvumilia au kumwondoa kazini.

Njia inayofaa ni kufanya mazungumzo ya faragha, kwa heshima na kwa mifano halisi.

Harvard Program on Negotiation inapendekeza kiongozi ataje tabia inayomsumbua, amruhusu mfanyakazi kueleza kinachoiendesha na ahakikishe ameelewa mtazamo wake kabla ya kutafuta suluhisho. Mazungumzo hayo yanaweza kufichua tatizo ambalo halikuwa linaonekana.

Badala ya kusema, "Wewe ni mvivu," kiongozi anaweza kusema: "Ripoti tatu zimechelewa wiki hii, na hali hiyo imecheleweesha kazi ya wengine. Kuna changamoto gani?" Kisha amsikilize mfanyakazi.

## Msaada uende sambamba na hatua

Baada ya kuelewa tatizo, kiongozi na mfanyakazi waweke makubaliano yanayoeleweka: Nini kinatakiwa kubadilika? Msaada gani utatolewa? Mabadiliko yanatarajiwa ndani ya muda gani? Maendeleo yatapitiwa lini?

Makubaliano yaandikwe inapofaa na yafuatiliwe. Kiongozi atoe mrejesho unaolenga tabia na matokeo, si kumshambulia mtu.

Iwapo tatizo linaendelea licha ya hatua stahiki, taasisi inaweza kutumia taratibu zake za kiutumishi na sheria zinazohusika, kwa haki na bila kufanya maamuzi ya jazba. Kulinda ustawi wa wafanyakazi wengine nako ni wajibu wa uongozi.

Hatimaye, kushughulikia mfanyakazi mwenye changamoto si kuchagua kati ya kumhurumia na kumwadhibu. Ni kutambua tatizo, kusikiliza, kutoa msaada, kuweka viwango na kusimamia uwajibikaji.

Kabla hujasema mfanyakazi ndiye tatizo, hakikisha umechunguza uwezo wake, mazingira yake, utayari wake—na nafasi yako mwenyewe katika tatizo hilo.

Kiongozi mzuri haharakishi kutoa hukumu. Anahakikisha kwanza ameelewa tatizo analotaka kulitatua.

# Miaka 9-12: Amri pekee haitoshi–mjenge kwa imani, mazungumzo na uwajibikaji

**MTOTO wa miaka tisa hadi 12 anaweza kuonekana bado mdogo, lakini anaanza kuingia katika kipindi cha mabadiliko muhimu. Anauliza maswali mengi, anataka kufanya baadhi ya mambo mwenyewe, anajali maoni ya marafiki na huenda akaanza kuona mabadiliko ya mwili yanayohusiana na kubalehe.**

**Mzazi anaweza kutafsiri hali hiyo kuwa ukaidi na kuongeza amri. Lakini wataalamu wa malezi wanaeleza kwamba mtoto wa umri huu bado anahitaji ukaribu wa wazazi, huku akijifunza kujitegemea hatua kwa hatua.**

**Katika malezi ya Kiislamu, huu ni wakati wa kuimarisha imani, ibada na tabia njema kwa kutumia maelezo, mfano wa wazazi na majukumu yanayolingana na umri.**

## Mruhusu kuuliza, msaidie kuelewa.

Mtoto anaweza kuuliza kwa nini anapaswa kuswali, kuvaa hijab au kufuata desturi fulani ambazo marafiki zake hawazifuati. Usichukulie kila swali kuwa dalili ya uasi.

Mweleze hukumu za dini kwa maarifa na ufafanue hekima yake kadiri anavyoweza kuelewa. Katika suala la hijab, kwa mfano, zungumza kuhusu staha, utu na ibada badala ya kutegemea vitisho pekee.

Qur'an inatuonesha mfano wa Luqman anayemnasihi mwanawe kwa upendo kuhusu imani, swala, subira na mwenendo mwema [Qur'an 31:13, 17–19]

Mtafiti wa malezi ya Kiislamu, Dk Hatem El Haj, anashauri watoto wa umri huu wafundishwe kwa mifano inayoonekana, maelezo rahisi na maswali yanayowachochea kufikiri. Hivyo, unapomfundisha ukweli, uaminifu au huruma, tumia matukio ya nyumbani, shuleni na katika jamii.

Usipolijua jibu la swali la kidini, sema utatafuta ufafanuzi kutoka kwa mtu mwenye elimu. Ni bora mtoto akuzoe kama sehemu salama ya kuuliza kuliko afiche maswali yake kwa kuogopa kukemewa.

## Imarisha ibada kwa kumjengea mazoea.

Katika kipindi hiki, msaidie mtoto kuanza kujikumbusha muda wa swala badala ya kusubiri kuitwa kila wakati. Pangeni shughuli za nyumbani kwa kuzingatia nyakati za ibada na salini pamoja inapowezekana.

Qur'an inahimiza familia kuamrishwa swala na kustahimili katika kulisimamia [Quran, 20:132).

Kumbuka kwamba kubalehe hutokea katika nyakati tofauti. Mtoto anapofikia baleghe, wajibu wa kidini unaohusika unakuwa wa lazima; hivyo maandalizi yaanze mapema, kwa elimu na uangalizi.

Qur'an nayo isomwe pamoja na maana. Mnaweza kuchagua aya moja na kujadiliana inavyohusiana na maisha ya kila siku. Msaidie mtoto kujifunza kwa kadiri ya uwezo wake, bila kumlinganisha na aliyefanikiwa kuhifadhi sehemu kubwa zaidi.

## Zungumzeni kuhusu marafiki na mabadiliko ya mwili.

Katika miaka hii, urafiki unapata umuhimu mkubwa. Mjue rafiki wa mtoto wako na familia yake inapowezekana. Mfundishe kutambua rafiki anayemshawishi kufanya mema na anayemshinikiza kufanya jambo hatari.

Usimdhihaki kwa kupenda marafiki; mpe pia nafasi ya kushiriki michezo na shughuli za jamii zenye manufaa.

Mueleze mapema, kwa heshima na kulingana na umri wake, mabadiliko ya kubalehe. Wavulana na wasichana wanahitaji kuelewa usafi wa mwili na masuala ya kidini yanayowahusu, ikiwamo kuoga janaba na, kwa wasichana, hedhi. Usimwache ajifunze kila kitu kwa marafiki au mitandao.

## Simu ije na mipaka, si marufuku pekee.

Kubalianeni kuhusu muda wa kutumia simu, programu zinazofaa na kutotuma picha au taarifa binafsi kwa watu wasioaminika. Mfundishe akueleze akitishwa, akidhalilishwa au akiombwa kuficha jambo linalomtia wasiwasi.

Heshimu faragha yake kwa kiwango kinacholingana na umri, huku ukitimiza wajibu wa kumlinda. Usigeuze uangalizi kuwa upekuzi wa kila mara bila sababu. Wazazi nao waoneshe mfano kwa kuacha simu wakati wa mazungumzo na watoto.

## Mpe majukumu na umjengee mahali pa kujisikia anakubalika.

Mzoeshe kupanga vifaa vya shule, kusaidia kazi za nyumbani, kutunza fedha kidogo na kuweka malengo. Sifia juhudi na maendeleo yake, si matokeo ya mitihani pekee.

Msaidie aipende familia, msikiti na jumuiya ya Waislamu. Msikiti usiwe mahali anapokemewa kwa kelele tu; uwe pia sehemu ya kujifunza, kupata marafiki wema na kuhisi anakubalika.

Weka sheria zilizo wazi na ueleze sababu zake. Mtoto akikosea, rekebisha kitendo bila kumdhalilisha au kumfanya aamini kwamba hana thamani.

Zaidi ya yote, tumia muda naye. Msikilize bila kugeuza kila mazungumzo kuwa hotuba. Ukiona mabadiliko makubwa yanayodumu katika hisia, usingizi, masomo au mahusiano yake, tafuta ushauri wa kitaalamu.

Miaka tisa hadi 12 ni kipindi cha kumwandaa mtoto kwa maamuzi atakayofanya bila uwepo wako.

Usimlee ili akutii unapomtazama tu. Mlee ili imani, maadili na uhusiano wenu vimwongoze hata usipokuwepo.

Na Samrath Msuya
0789 201 383

# Ubunifu katika ufundishaji hisabati

## SEHEMU YA 3

## Hesabu haikai darasani: Ipo katika maisha yetu kila siku

**Mtoto anaweza kutoka darasani akiwa na daftari lililojaa kanuni za hesabu, lakini bado akashindwa kuona uhusiano kati ya alichojifunza na maisha yanayomzunguka. Anaweza kujua namna ya kuhesabu asilimia, lakini asitambue kwamba punguzo la bei dukani ni suala la asilimia. Anaweza kujua vipimo, lakini asione uhusiano wake na kupika, kujenga au kupanga eneo la bustani.**

**Hapo ndipo kuna changamoto nyingine katika ufundishaji wa hisabati. Somo linapobaki kwenye namba, alama na kanuni pekee, linaweza kuonekana kama jambo la darasani ambalo lengo lake kubwa ni kupita mtihani. Lakini kwa kweli, hesabu iko karibu kila mahali tunapoishi.**

**Tunaitumia tunapopanga matumizi ya fedha, tunapofanya biashara, tunaponunua sokoni, tunapopima muda wa safari, tunapojenga, tunapopika, tunapolinganisha bei na tunapochambua taarifa mbalimbali. Hata mtu anayesema "mimi situmii hesabu" mara nyingi anaitumia bila kutambua.**

### Kutoka kwenye kanuni kwenda kwenye maisha

Wataalamu wa elimu ya hisabati wanahimiza wanafunzi wasijifunze kanuni pekee, bali waone namna maarifa hayo yanavyotumika kuelewa na kutatua matatizo halisi. Njia hiyo humsaidia mtoto kuunganisha kile anachojifunza darasani na mazingira yake.

Kwa mfano, hesabu ya kugawanya inaweza kuhusishwa na kugawa bidhaa katika vifurushi, kupanga watu kwenye magari au kugawana kitu kwa uwiano. Hesabu haijabadilika, lakini mtoto sasa anaona sababu ya kuitumia. Hilo ni muhimu kwa sababu matatizo ya maisha hayaji yakiwa yameandikwa pembeni: "Tumia kuzidisha" au "Tumia asilimia." Mtu mwenyewe ndiye anayepaswa kutambua ni maarifa gani ya kihesabu yanayohitajika.

### Sokoni nako kuna hesabu

Mzazi anaweza kumsaidia mtoto kujifunza hesabu hata bila kukaa naye mezani na kitabu. Akienda naye sokoni, anaweza kumuuliza kiasi cha fedha walichonacho, watakachotumia na watakachobakiwa nacho. Anaweza pia kumuuliza bidhaa ipi ni nafuu zaidi au gharama itabadilika vipi wakiongeza kiasi wanachonunua.

Nyumbani pia kuna hesabu nyingi. Kuna vipimo, muda, tarehe, bajeti na mgawanyo wa vitu. Uwanjani kuna alama, muda na takwimu; kwenye biashara kuna gharama, mapato, faida na hasara; na kwenye ujenzi kuna urefu, upana, eneo na kiasi cha vifaa kinachohitajika.

Mazungumzo hayo hayahitaji kugeuzwa kuwa mtihani. Lengo ni kumsaidia mtoto kuona kuwa hesabu anayoiona kwenye daftari inaishi katika mazingira yake. Kadiri anavyoona uhusiano huo, ndivyo somo linavyoweza kuanza kuwa na maana zaidi kwake.

### Mtoto aione hesabu iliyojificha kwenye tatizo

Vitabu vya hesabu vina nafasi muhimu katika kujifunza, lakini mazingira yanayotuzunguka nayo yanaweza kuwa sehemu ya somo. Badala ya kila mara kuanza na kanuni, wakati mwingine mwalimu anaweza kuanza na hali ya kawaida na kuuliza: "Kuna hesabu gani hapa?"

Swali hilo linamtaka mwanafunzi aangalie, afikiri na kutambua tatizo kabla hajakimbilia kwenye kanuni. Tafiti kuhusu ubunifu katika hesabu zinaonyesha umuhimu wa kuwapa wanafunzi nafasi ya kuchunguza matatizo, kujaribu njia mbalimbali na kueleza mawazo yao.

Hii ndiyo sababu mazingira ya mtoto yanaweza kuwa nyenzo nzuri sana ya kujifunzia. Shule iliyopo katika eneo la biashara inaweza kutumia mifano ya biashara; eneo la kilimo linaweza kutumia mavuno, vipimo na maeneo ya mashamba; huku mazingira ya mijini yakitoa mifano ya usafiri, majengo, biashara na matumizi ya fedha.

### Wazazi nao wana nafasi

Mjadala wa ufundishaji wa hesabu usimwangalie mwalimu pekee. Wazazi wana nafasi kubwa ya kumsaidia mtoto kuona hesabu katika maisha ya kawaida. Si lazima mzazi awe mtaalamu wa hisabati; anaweza kumshirikisha mtoto katika kupanga matumizi, kulinganisha bei, kupima vitu au kukadiria muda.

Muhimu zaidi, anaweza kumzoesha mtoto kufikiri. Badala ya kuuliza tu kama jibu ni sahihi, wakati mwingine anaweza kuuliza, "Umejuaje?" au "Umefikaje hapo?" Maswali madogo kama hayo yanaweza kumsaidia mtoto kuona kuwa hesabu si kutafuta jibu pekee, bali pia kuelewa namna ya kulifikia.

### Hesabu ni chombo cha kuelewa dunia

Tunapowafundisha watoto hesabu kama orodha ya kanuni za kukariri, tunaweza bila kukusudia kuwaficha sehemu yake inayovutia zaidi. Hesabu imetusaidia kujenga majengo, kupanga biashara, kuelewa sayansi, kutengeneza teknolojia na kufanya maamuzi katika maisha ya kawaida.

Kwa hiyo, mtoto asijifunze tu kwamba asilimia ni nini. Aone asilimia katika maisha. Asijifunze vipimo pekee. Aone vipimo vinavyofanya kazi. Asifanye takwimu kwa sababu zipo kwenye mtihani tu; aanze kuona namna takwimu zinavyosaidia kuelewa jambo. Hapo ndipo hesabu inaanza kuwa na maana.

Na pengine mtoto anayejua hesabu inatumiwa wapi atakuwa na sababu kubwa zaidi ya kutaka kujua jinsi inavyofanya kazi.

Katika makala ijayo tutahitimisha mfululizo huu kwa kuangalia njia rahisi ambazo mwalimu anaweza kuanza nazo ili kufanya darasa la hesabu liwe na uhai zaidi, bila kuhitaji vifaa vya gharama kubwa wala kubadilisha mtaala mzima.

Na Junaynat Ally Dama

# Uandishi wa habari kwa msaada wa AI

SEHEMU YA 3

## AI katika kukusanya taarifa: Inawezaje kusaidia utafiti, vyanzo na mahojiano?

**Baada ya kupata wazo na kuchagua mwelekeo wa habari, kazi inayofuata ndiyo inayotenganisha wazo na habari halisi: kukusanya taarifa. Mwandishi anahitaji kujua historia ya suala analolifuatilia, kutafuta nyaraka, kubaini watu wa kuzungumza nao, kuandaa maswali na kulinganisha majibu anayopata.**
**Hapa pia akili bandia (AI) inaweza kuokoa muda na kumsaidia mwandishi kujiandaa vizuri. Lakini mpaka wake lazima uwe wazi tangu mwanzo: AI inaweza kusaidia katika utafiti; haiwezi kuchukua nafasi ya chanzo.**

### Anza kwa kuelewa jambo unalokwenda kuripoti

Fikiria umepewa taarifa ya kwenda kumhoji mtaalamu kuhusu mabadiliko mapya ya kodi, sheria, hali ya uchumi au mradi mkubwa wa Serikali. Huenda una muda mfupi wa kujiandaa na mada yenye maneno mengi ya kitaalamu.

AI inaweza kusaidia kupata picha ya awali. Unaweza kuiomba ikuelezee dhana fulani kwa lugha rahisi, ikusaidie kutambua masuala makuu yanayohusiana nayo au ikutengenezee maneno muhimu ya kutumia unapotafuta taarifa zaidi..

Hapa lengo si kuchukua maelezo ya AI na kuyachapisha. Lengo ni kujijengea uelewa wa kuanzia, ili ujue unachopaswa kutafuta katika vyanzo vinavyoaminika.

Kwa mfano, badala ya kuuliza, "Nieleze kila kitu kuhusu sukuk," mwandishi anaweza kuuliza: "Ninajiandaa kufanya habari kuhusu sukuk. Nitajie dhana muhimu ninazopaswa kuelewa na maswali ambayo ninapaswa kuyafanyia utafiti zaidi."

Baada ya hapo, anapaswa kwenda kwenye sheria, ripoti, taasisi husika, wataalamu na vyanzo vingine halisi.

### AI inaweza kusaidia kutafuta vyanzo vya aina gani vinahitajika

Habari nzuri haijengwi kwa kuzungumza na mtu mmoja tu. Mara nyingi mwandishi anahitaji mamlaka inayohusika, mtaalamu, mtu aliyeathirika, takwimu na wakati mwingine upande unaopinga au kuhoji madai yaliyotolewa.

AI inaweza kusaidia katika kile kinachoweza kuitwa ramani ya vyanzo. Mwandishi anaweza kueleza habari anayofuatilia na kuuliza ni aina gani za watu, taasisi au nyaraka zinapaswa kuhusishwa.

Tuseme unaandaa habari kuhusu ongezeko la ada katika huduma fulani. AI inaweza kukukumbusha kufikiria mamlaka inayosimamia huduma hiyo, mtoa huduma, watumiaji, wataalamu wa uchumi au sheria na nyaraka zinazoonesha mabadiliko ya gharama.

Lakini kuna tofauti muhimu. AI inaweza kupendekeza aina ya chanzo; usiamini moja kwa moja jina, cheo, namba ya simu au taasisi inayokutajia bila kuthibitisha.

### Jiandae vizuri kabla ya mahojiano

Mwandishi mwenye maandalizi mazuri ana nafasi kubwa ya kufanya mahojiano mazuri.

AI inaweza kusaidia kutengeneza orodha ya awali ya maswali. Ukiieleza mada, mtu unayekwenda kumhoji na jambo unalotaka kufahamu, inaweza kukupendekezea maeneo ya kuuliza.

Hii ni muhimu hasa pale ambapo mwandishi anaogopa kusahau jambo muhimu. Lakini maswali ya AI yasichukuliwe kama dodoso la lazima la kufuata kutoka mwanzo hadi mwisho.

Mahojiano mazuri yanaishi. Chanzo kinaweza kusema jambo ambalo hukutarajia. Mwandishi anatakiwa kulisikiliza na kuuliza swali la kufuatilia. Hapo uzoefu, umakini na udadisi wa mwandishi ni muhimu kuliko orodha yoyote iliyotengenezwa kabla ya mahojiano.

Kwa hiyo, AI inaweza kukusaidia kuingia kwenye mahojiano ukiwa umejiandaa. Haiwezi kukusikilizia chanzo.

### Itumie kutafuta maswali ambayo hukuyafikiria

AI inaweza kuwa na manufaa zaidi ukiitumia kujaribu maandalizi yako. Baada ya kutengeneza maswali yako mwenyewe, unaweza kuiuliza: "Ni maswali gani muhimu kuhusu suala hili ambayo yanaonekana kukosekana katika orodha yangu?"

Au: "Ni madai gani ambayo chanzo hiki kinaweza kutoa ambayo nitahitaji kuyaomba ushahidi?" Hapo AI haichukui nafasi ya mwandishi. Inatumika kama mtu wa pili anayepitia maandalizi yako na kukusaidia kuona pengo.

Hata hivyo, si kila swali linalopendekezwa litakuwa zuri. Baadhi yanaweza kuwa ya jumla, yasiyoendana na mazingira ya Tanzania au hata kujengwa juu ya dhana isiyo sahihi. Mwandishi ndiye anayechuja.

### Baada ya mahojiano, inaweza kusaidia kupanga kazi

Mahojiano ya dakika 45 yanaweza kumwachia mwandishi sauti ndefu na dondoo nyingi. AI inaweza kusaidia kubadili sauti kuwa maandishi, kupanga mada zilizojadiliwa au kutoa muhtasari wa maeneo makuu.

Inaweza pia kusaidia pale mahojiano yamefanyika kwa lugha tofauti, kwa kutoa tafsiri ya awali ambayo mwandishi anaweza kuipitia.

Lakini hapa kuna kanuni muhimu sana: nukuu lazima ihakikiwe dhidi ya sauti halisi. AI inaweza kusikia neno vibaya, kuchanganya majina au kubadili maana ya sentensi. Kwa habari yenye nukuu nyeti, tofauti ya neno moja inaweza kubadili maana kabisa. Kwa hiyo, maandishi yanayotengenezwa na AI ni msaada wa kazi. Si ushahidi wa mwisho wa alichosema chanzo.

Na Junaynat Ally Dama

# Macho yako ni hazina: Tabia 10 zitakazolinda uono

**MACHO hutuwezesha kusoma, kufanya kazi, kuendesha vyombo vya usafiri na kutambua mazingira yanayotuzunguka. Hata hivyo, wengi wetu huyakumbuka tunapoanza kuona ukungu, kupata maumivu au kushindwa kusoma maandishi madogo.**

**Baadhi ya mabadiliko ya kuona huambatana na umri, lakini si sahihi kudhani kwamba kupoteza uwezo wa kuona ni jambo lisiloepukika. Magonjwa kadhaa yanaweza kugunduliwa na kutibiwa mapema, na tabia nzuri zinaweza kupunguza hatari ya matatizo mengine.**

**Haya ni mambo kumi muhimu ya kuzingatia.**

**_Kwanza,_ pima macho hata kama unaona vizuri.**

Magonjwa kama glakoma, mtoto wa jicho, matatizo ya retina yanayohusiana na umri na madhara ya kisukari yanaweza kuanza bila dalili zinazotambulika kirahisi. Uchunguzi wa macho unaweza pia kugundua matatizo ya kuona karibu au mbali. Kwa watu wengi wazima, uchunguzi kila mwaka mmoja hadi miwili ni mwongozo wa jumla, lakini daktari anaweza kushauri vinginevyo. Jua kama ndugu wana historia ya magonjwa ya macho, mjulishe mtaalamu.

**_Pili,_ linda macho dhidi ya mionzi ya jua.**

Mionzi ya ultraviolet (UV) inaweza kusababisha matatizo ya macho. Tumia miwani inayozuia mionzi ya UVA na UVB na si lazima iwe ghali; muhimu ni uwezo wake wa kutoa kinga. Kofia yenye ukingo mpana husaidia pia. Usisubiri jua kali pekee. Kinga inahitajika hata siku zenye mawingu. Watoto nao walindwe wanapocheza nje.

**_Tatu,_ kula vyakula vinavyosaidia afya ya macho.**

Lishe bora inapaswa kuwa na vitamini A, C na E, pamoja na virutubisho vya lutein na zeaxanthin, vinavyopatikana hasa katika mboga za majani. Vitamini A ni muhimu kwa uwezo wa kuona katika mwanga hafifu, huku virutubisho vingine vikisaidia kulinda seli za macho. Jumuisha mchicha, karoti, viazi vitamu, machungwa, parachichi, karanga, mbegu na samaki wenye mafuta, kama dagaa na sardini. Samaki wana omega-3,

**_Nne,_ kunywa maji ya kutosha.**

Upungufu wa maji huchangia macho kuwa makavu na yenye muwasho. Jenga utaratibu wa kunywa maji kulingana na mahitaji yako, hali ya hewa na ushauri wa kitabibu. Wanaofanya kazi kwenye viyoyozi au kutumia skrini kwa muda mrefu wanapaswa kuzingatia pia dalili za ukavu wa macho.

Iwapo tatizo linaendelea, mtaalamu anaweza kupendekeza matone maalumu ya kuongeza unyevu (artificial tears). Usijitibu kwa matone yoyote bila kujua chanzo cha tatizo.

**_Tano,_ fanya mazoezi na dhibiti magonjwa sugu.**

Mazoezi ya mara kwa mara na uzito unaofaa husaidia kupunguza hatari ya matatizo ya kiafya yanayoweza kuathiri macho. Kisukari kisichodhibitiwa kinaweza kuharibu mishipa ya damu katika retina. Shinikizo la damu na kiwango kikubwa cha mafuta kwenye damu navyo vinahitaji kudhibitiwa. Tumia dawa ulizoelekezwa, fuatilia vipimo, kula vizuri na fanya mazoezi.

**_Sita,_ punguza uchovu unaotokana na skrini.**

Kutazama simu, kompyuta au televisheni kwa muda mrefu kunaweza kusababisha macho kukauka, kuona ukungu, maumivu ya kichwa na uchovu. Tunapokazia macho skrini, huwa tunapepesa macho mara chache zaidi.

Tumia kanuni ya 20–20–20: kila baada ya dakika 20, angalia kitu kilicho umbali wa futi 20, takribani mita sita, kwa sekunde 20. Pepesa macho mara kwa mara. Rekebisha mwangaza na urefu wa skrini, kaa katika mkao unaofaa na punguza mwanga unaoakisiwa kwenye skrini.

**_Saba,_ acha sigara na pombe**

Uvutaji sigara huongeza hatari ya mtoto wa jicho, ugonjwa wa retina unaohusiana na umri na madhara kwenye neva ya macho. Kuacha sigara hupunguza hatari za kiafya, hata kwa mtu aliyevuta kwa muda mrefu. Unywaji mwingi wa pombe nao unapaswa kuepukwa.

**_Nane,_ jikinge dhidi ya majeraha, zing**atia usafi.

Tumia miwani maalumu ya kujikinga unapochomelea, kukata vitu, kufanya ukarabati, kushughulika na kemikali au kucheza michezo yenye hatari ya kugongwa machoni.

Epuka kusugua macho kwa mikono michafu. Tabia hiyo inaweza kuongeza muwasho, kuingiza vijidudu na kuathiri konea. Ondoa vipodozi vya macho kabla ya kulala na usishirikiane na wengine vipodozi hivyo.

UKHTI FATIMA SS

# Wakati mwingine huhitaji kujibadili, unahitaji kubadili mazingira uliyopo

**KUNA mtu anajilaumu kila siku kwa kushindwa kutimiza malengo yake. Anajiona mvivu kwa sababu hasomi vitabu alivyonunua, hana nidhamu kwa sababu hapigi hatua kazini, au hana uvumilivu kwa sababu kila anaporudi nyumbani anajikuta amechoka na mwenye hasira. Anajaribu kujibadili. Anaweka ratiba mpya, anaahidi kuongeza bidii na kujikemea kila anaposhindwa. Lakini matokeo yanabaki yale yale. Huenda swali analopaswa kujiuliza si, "Kwa nini mimi ni dhaifu?" Bali, "Je, mazingira yangu yananisaidia au yananifanya kila kitu kiwe kigumu zaidi?"**

**Katika saikolojia, mazingira si nyumba, ofisi au mtaa pekee. Yanajumuisha pia watu tunaoshirikiana nao, utamaduni, mifumo ya taasisi na hali zinazotuzunguka. Mwanasaikolojia Kurt Lewin alisisitiza kwamba tabia ya mtu inapaswa kueleweka kwa kuangalia mwingiliano kati yake na mazingira yake.**

**Hii haimaanishi kwamba hatuwajibiki kwa matendo yetu. Inamaanisha hatupaswi kujichunguza wenyewe huku tukipuuza mazingira yanayotushawishi, kutuchosha au kutuzuia.**

## Mazingira yanaweza kufanya jambo dogo liwe gumu

Fikiria mwanafunzi anayeamua kusoma kwa saa mbili kila jioni. Lakini anasomea sebuleni ambako televisheni inawaka, watu wanazungumza na simu yake inapokea taarifa kila baada ya dakika chache.

Akishindwa kuzingatia masomo, anaweza kujilaumu kwamba hana nidhamu. Lakini akihamia sehemu tulivu, akazima taarifa za simu na kuweka vitabu karibu, huenda kazi ileile ikawa rahisi zaidi. Hajabadilisha uwezo wake wa kufikiri. Amebadilisha mazingira yanayohitaji nguvu zake za umakini.

Maandishi ya Sara Lindberg, yaliyopitiwa kitabibu na daktari wa magonjwa ya akili Akeem Marsh, yanaeleza kwamba kelele, mwanga, mpangilio wa vitu na mazingira ya kijamii vinaweza kuathiri umakini, hisia na kiwango cha msongo wa mawazo.

Kwa hiyo, wakati mwingine suluhisho si kuongeza nguvu ya kujizuia. Ni kupunguza vitu vinavyokulazimisha kujizuia kila dakika.

Unataka kupunguza muda wa kutumia simu? Usiiweke pembeni ya kitanda unapolala. Unataka kuanza mazoezi? Andaa vifaa mapema. Unataka kusoma? Tengeneza sehemu inayokukumbusha kusoma badala ya kukupeleka kwenye mambo mengine. Mabadiliko madogo ya mazingira yanaweza kufanya tabia unayoitaka iwe rahisi zaidi kuitekeleza.

## Wakati mwingine mazingira yenyewe yana madhara

Lakini si kila tatizo linahusu meza yenye vitu vingi au simu inayosumbua. Kuna mazingira yanayochosha mtu kwa sababu ya namna anavyotendewa.

Fikiria mfanyakazi anayefanya kazi katika ofisi ambayo kila kosa linajibiwa kwa matusi. Hakuna anayesikiliza maoni yake. Anapewa majukumu mengi bila msaada, na hata akifanya vizuri hakuna anayethamini mchango wake.

Anaweza kuambiwa kila siku: "Badilisha mtazamo. Jifunze kuwa mvumilivu. Ongeza bidii." Lakini je, tatizo ni mtazamo wake pekee?

Mazingira ya kazi yenye unyanyasaji, msongo mkubwa, ukosefu wa msaada na hisia za kutothaminiwa yanaweza kuathiri ustawi wa akili. Vivyo hivyo, migogoro ya kudumu na mahusiano yanayomnyima mtu hali ya usalama yanaweza kuongeza msongo. Hapa ndipo tunapopaswa kuwa makini na ushauri wetu.

Si kila anayechoka anahitaji kuambiwa avumilie zaidi. Si kila anayepoteza hamasa anahitaji hotuba ya nidhamu. Wakati mwingine anahitaji mazingira yenye heshima, msaada, usalama au nafasi ya kukua.

Na si lazima mazingira yenye madhara yawe ofisini. Yanaweza kuwa katika kundi la marafiki wanaokatisha tamaa kila wazo lako, nyumbani penye migogoro isiyoisha au kwenye mitandao inayokufanya ujilinganishe na wengine kila siku.

Neno sumu hapa ni taswira ya mazingira yanayokuathiri kwa namna ya kudumu, si utambuzi wa kitabibu wala sababu ya kumhukumu kila mtu ambaye hamuelewani.

## Ubadili mazingira au ujibadili? Jibu linahitaji busara.

Kabla ya kuchukua uamuzi mkubwa, chunguza ni wakati gani unajisikia umechoka, umeshindwa kuzingatia au umepoteza hamasa. Ni vitu gani vinavyojirudia? Hali yako inabadilikaje unapokuwa sehemu nyingine au unapokuwa na watu wengine?

Jaribu kurekebisha yale yaliyo ndani ya uwezo wako. Punguza usumbufu, panga upya mahali pa kazi, weka mipaka kwenye matumizi ya simu, tafuta watu wanaokutia moyo au zungumza kuhusu mazingira yanayokukwaza.

Lindberg anashauri kuanza na mabadiliko madogo yanayowezekana na kuangalia kama yanaleta tofauti kabla ya kufanya uamuzi mkubwa wa kubadili mazingira. Anaeleza pia kwamba kuhama au kubadili kazi si jambo linalowezekana kwa kila mtu. Ikiwa mazingira yana unyanyasaji au yanahatarisha usalama wako, tafuta msaada wa watu unaowaamini na huduma zinazofaa. Hupaswi kujilazimisha kubaki kwenye hatari kwa jina la kujenga uvumilivu.

Vilevile, kubadili mazingira hakutatui kila tatizo la afya ya akili. Wakati mwingine msaada wa kitaalamu bado unahitajika.

Hatimaye, kujiboresha ni jambo muhimu. Nidhamu, uvumilivu na bidii vina nafasi yake. Lakini maendeleo hayahitaji kila wakati kujilazimisha zaidi.

Kabla hujahitimisha kwamba wewe ndiye tatizo, jiulize kama mazingira yako yanakupa nafasi ya kuwa mtu unayetaka kuwa.

Wakati mwingine hatua kubwa ya kujibadili huanza kwa kubadili mazingira yanayokuzunguka.